# Nipashe

Jumatano Mei 22, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581684

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**WABUNGE** watoa angalizo wenyeji kukosa fursa Soko la EAC Ubungo

UKURASA 3

**MAKONDA** aanza ziara kupembua mbivu na mbichi

UKURASA 5



**RAIS** wa Iran kuzikwa leo, Kaimu Rais asema hakuna cha kuharibika

UKURASA 19



**ANGE ATAKA WATATU SPURS**

UKURASA 22

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### WALAZWA BAADA YA KUMWAGIWA KEMIKALI

WATU wanne wa familia moja wamelazwa katika Hospitali ya Rufani...

UKURASA WA 8

RIPOTI MAALUM

### MAISHA MAPYA YA WENYEJI MTO UKIVAMIA MAKAZI YAO

ATHARI za mabadiliko ya tabianchi hivi sasa zinaonekana dhahiri. Angalia maisha mapya ya wakazi wa Mabibo...



**Profesa Mukandala: MV Bukoba ilikuwa 'bomu' tangu ununuzi wake**

UKURASA 5



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi.

BAADA YA ASKOFU...

# Frateri wa Katoliki adaiwa kujinyonga

**Aning'inia** kwenye mshipi; mwanasaikolojia asema kitendo hicho hakina mwenyewe...

*Endelea ukurasa wa 2*

# Jenereta la hospitali ladoda mwaka mzima kwa kukosa lita 15 za dizeli



**Na Vitus Audax**

JENERETA lililotolewa na Wizara ya Afya kwa Hospitali ya Wilaya ya Busega mkoani Simiyu kwa zaidi ya mwaka mmoja halijatumika kutokana na kukosa kilo tano za chumvi, makopo mawili ya mkaa na lita 15 za dizeli.

Hali hiyo imesababisha kukwama kwa shughuli za kitabibu hospitalini hapo hususani umeme unapokatika, hivyo kuwalazimu kusubiri urejee.

Suala hilo liliibuliwa jana wakati wa ziara...

ENDELEA UK 2

**MICHEZO** SHAHIDI WA DSTV AITAJA WIZARA KESI MADAI DITTO UK 23

MAONI, KATUNI UK.6

# Frateri adaiwa kujinyonga kwa mshipi

**Na Romana Mallya**

MATUKIO ya watumishi wa Mungu kujinyonga yanaongezeka huku mwanasaikolojia na mtaalam wa afya wakitaja kinachochangia uamuzi huo ugumu wa maisha na kushindwa kufikia malengo.

Aidha, Mtaalam wa afya amesema kuwa daktari, mtumishi wa Mungu, Rais na yeyote hawana kinga dhidi ya magonjwa ya akili na kuumwa magonjwa hayo haitegemei kiwango cha uchamungu au wadhifa.

Hayo yanakuja baada ya Frateri wa Kanisa Katoliki Shirika la Roho Mtakatifu Jimboni Tanga, Rogassion Hugho (25), anadaiwa kujinyonga hadi kufa katika nyumba yao ya malezi mkoani humo, huku sababu ikidaiwa ni kufeli mitihani ya kwenda hatua ya ushemasi.

Tukio hilo limetokea baada ya lile lililotokea Mei 16, mwaka huu, jijini Dodoma la Askofu Mkuu wa Kanisa la Methodist, Joseph Bundala, kudaiwa kujinyonga ndani ya ofisi yake iliyoko katika kanisa hilo eneo la Meriwa kwa kile kinachodaiwa kuwa ni madeni na mgogoro wa uendeshaji wa shule binafsi.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga, Almachius Muchunguzi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi, huku akisema frateri huyo alitumia mshipi kutekeleza tukio hilo.

Katika tukio hilo, Kamanda Muchunguzi alisema amejinyonga kwa kutumia mshipi (unaofungwa kiunoni) katika nyumba yao ya Malezi ya Magamba aliyokuwa akiishi.

"Tukio hili ni la kweli limetokea jana (juzi). Amejinyongea kwenye makazi yao ambayo wanajiandaa kuwa mapadri. Sababu ya mwanzo inayosemekana ni kwamba kawaida hufanya mitihani kwenda hatua nyingine sasa akawa amefeli.

"Ninasikia hakukubaliana na hiyo hali ya kushindwa, akapata msongo wa mawazo na akaona njia bora afanye hivyo. Amejinyonga kwa kutumia kamba hizi wanazojifunga kiunoni (mshipi)," alisema.

Aprili 12, 2022, Paroko wa Parokia Mt. Yohanne Paul II, Mbezi Mshikamano, Francis Kangwa, alifariki dunia na mwili wake kukutwa kwenye tangi la maji nyuma ya nyumba ya mapadri wa Shirika la Missionaries of Africa iliyoko Kanisa Kuu la Mtakatifu Joseph, Dar es Salaam.

**MWANASAIKOLOJIA**

Mwanasaikolojia-Tiba Saldin Kimangale, alisema siku za hivi karibuni kumekuwapo matukio kadhaa ya watumishi wa dini kusitisha uhai wao, huku sababu zikitajwa ugumu wa maisha na kushindwa kufikia malengo.

"Bila shaka hizi ni sababu za kuwezesha mazungumzo yaendelee na kufunga kurasa za mijadala. Asilimia takriban 60 ya watanzania wanaishi kwenye umaskini uliotopea, achilia mbali kufikia malengo mbalimbali.

"Ukweli ni kuwa nyuma ya mtu kusitisha uhai kuna mengi tusiyoyajua, yeyote anayesitisha uhai hakuanza kusitisha uhai wake siku ile aliyokamata kifaa cha kusitishia uhai na kusitisha, bali ni mchakato umeanza siku kadhaa nyuma hata miezi hata miaka," alisema.

Kimangale kutoka Kituo cha Somedics Polyclinic Heath Centre, Upanga, Dar es Salaam, alisema ifahamike kuwa daktari, mtumishi wa Mungu, Rais na yeyote hawana kinga dhidi ya magonjwa ya akili na kuumwa magonjwa hayo haitegemei kiwango cha uchamungu au wadhifa.

"Huu ni ugonjwa kama yalivyo magonjwa mengine yanampata mtu yeyote maadam yupo kwenye vihatarishi.

"Linapokuja suala la "Mtumishi wa Mungu" inaleta shida zaidi kwa sababu wao ndiyo hutarajiwa wawe na uvumilivu, subira, na uthabiti zaidi, na pia wawe na mbinu bora zaidi za mawasiliano na stadi za kutatua changamoto na matatizo mbalimbali kuliko watu wengine kwa kuwa jamii inawategemea," alifafanua.

Alisema dhana hiyo ya kuchukuliwa kuwa 'anapaswa kuwa hivi' ndiyo inayowafanya pengine wasizifikie huduma kwa dhana kuwa, wataonekana ni dhaifu au hawana imani na uchamungu.

Alisema watumishi wa Mungu kama wanadamu wengine wanapitia yale yale wanayopitia watu wa kawaida ikiwamo aibu, hatia na kujihisi kushindwa.

"Ni vyema kada hii itazamwe upya tena kimfumo, janga la watumishi wa Mungu halina tofauti sana na janga la wanaume wanaokabiliwa na taboo zinazowafanya wasilie nakutafuta msaada, sasa iwapo mtumishi ni mwanamume basi janga lake linakuwa kubwa zaidi.

"Sababu walizozitoa zina maana kubwa sana kwao, jamii lazima iziheshimu nakuzitumia kama angalizo, ugumu wa maisha nakutofikia malengo kwa mtu mmoja sio lazima iwe na maana sawa na mtu mwingine, ili tuweze kuwasaidia ipo haja ya kuwasikiliza na kuwasaidia kutatua changamoto zao," alisema.

Mwanasaikolojia huyo alisema kupewa kila kitu kinachowezesha maisha ya mtu haimaanishi ndiyo kufikia malengo, wapewe nafasi pia, kufikia vipawa vyao iwapo watapenda kufanya hivyo.




Makamu Askofu Mkuu wa Tanzania Methodist Church (TMC), Samuel Nyanza akiaga mwili wa aliyekuwa Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Joseph Bundala nyumbani kwake Ihumwa jijini Dodoma juzi, kabla ya mazishi yake yaliyofanyika katika kanisa la TMC Ihumwa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Serikali kuhamia Dodoma kuhitimishwa rasmi 2025

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema safari ya kuhamia Dodoma inatarajiwa kukamilika baada ya mpango kazi maalum na ujenzi wa awamu ya pili wa majengo ya ofisi za wizara na taasisi utakapohitimishwa mwaka 2025.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Bahi (CCM), Keneth Nollo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini zoezi la kuhamia Dodoma litakamilika na ni taasisi ngapi zimeshahamia Dodoma.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Nderiananga alisema hadi sasa watumishi wa umma 25,039 huku taasisi zilizohamia zikiwa ni 65.

Alifafanua kuwa shughuli ya kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma lilianza rasmi mnamo mwaka 2016.

Katika maswali ya nyongeza, Nollo alihoji ni lini mwisho kabisa wa taasisi za serikali kuhamia na ujenzi wa makazi rasmi viongozi utaanza lini.

Akijibu maswali hayo, Nderiananga alisema wanaendelea na uchambuzi na taarifa itakapokamilika watawaambia wabunge ni taasisi ngapi zimehamia na ngapi zimebaki na inatarajiwa Mwaka wa 2025 watakuwa wamehamia jijini Dodoma.

Kuhusu nyumba za viongozi, alisema kuanzia mwaka 2021/22 kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), walijenga nyumba 20, lakini Septemba 23 mwaka 2023 Makamu wa Rais alizindua nyumba 150.

Alisema wapo katika zoezi la kupanga eneo ambalo watalitwaa kwa ajili ya kujenga nyumba za viongozi wa serikali na watumishi la ekari 4,654 katika eneo la Mtumba na Ikulu.

# Jenereta la hospitali ladoda mwaka mzima kwa kukosa lita 15 za dizeli

**Na Vitus Audax**

JENERETA lililotolewa na Wizara ya Afya kwa Hospitali ya Wilaya ya Busega mkoani Simiyu kwa zaidi ya mwaka mmoja halijatumika kutokana na kukosa kilo tano za chumvi, makopo mawili ya mkaa na lita 15 za dizeli.

Hali hiyo imesababisha kukwama kwa shughuli za kitabibu hospitalini hapo hususani umeme unapokatika, hivyo kuwalazimu kusubiri urejee.

Suala hilo liliibuliwa jana wakati wa ziara ya kushtukiza hospitalini hapo, iliyofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Newanda, hivyo kutoa siku tano lianze kufanya kazi mara moja.

Dk. Nawanda aliwataka Mkuu wa Wilaya hiyo, Faidha Salim na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Michael Kachoma, kuhakikisha genereta hilo linaanza kazi haraka iwezekanavyo.

Mkuu huyo wa mkoa alishangazwa na uongozi wa hospitali hiyo kushindwa kugharamia vitu hivyo ambavyo havina gharama kubwa huku vitu vingine vilivyohitajika kufanikisha hatua hiyo vikitajwa kuwa ni pamoja na nyaya mbalimbali ambazo awali wataalamu walidai zinagharimu zaidi ya Sh. milioni 20.

"Taarifa nilizo nazo ni kuwa awali wataalamu walileta bajeti ya zaidi ya Sh. milioni 20. Baadaye ikapungua hadi Sh. milioni 18. Alipokuja mkurugenzi mpya ikapungua tena hadi Sh. milioni nne lakini taarifa zilizopo inaweza kupungua hadi laki nne," alisema.

Dk. Nawanda alisema Wizara ya Afya ilitoa jenereta hilo kwa ajili ya kusaidia huduma za upasuaji kwa wajawazito, watoto na watu wengine pindi umeme unapokatika.

"Ikifika hiyo tarehe 25 mwezi huu kabla halijaanza kufanya kazi, mkuu wa wilaya na mkurugenzi mtakuwa hamtoshi hapa. Haiwezekani mwaka mzima chumvi kilo tano, mkaa makopo mawili na lita 15 za dizeli mnashindwa," alisisitiza Dk. Nawanda.

Baada ya maagizo hayo, Kachoma alimhakikishia mkuu huyo wa mkoa kuwa ifikapo tarehe iliyotolewa litakuwa tayari limeanza kufanya kazi ili kukabiliana na adha ya utoaji huduma pindi umeme unapokatika.

# Wabunge watoa angalizo wenyeji kukosa fursa Soko la EAC Ubungo

**Na Jenifer Gilla**

WABUNGE wameshauri serikali kuhakikisha Kituo cha Biashara Afrika Mashariki hauumizi wafanyabiashara wa ndani kwa kuwabana wageni kufanya biashara ndogo.

Pia, wameshauri serikali kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo nchini ikiwamo mifumo rafiki ya kibenki na Mamlaka ya Mapato (TRA) ili kuwavutia wengi.

Akichangia hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2024/25, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga, Mwanaisha Ulenge, alishauri serikali kuhakikisha makubaliano wanayoingia na wafanyabiashara wa kigeni hasa kutoka China kuhusu utekelezaji mradi wa soko hilo, hayaathiri biashara ndogo zinazofanywa na wazawa.

Alisema wafanyabiashara wa China licha ya mikataba yao kuwatambua kuwa ni wa jumla, wamekuwa wakiuza pia kwa rejareja na kusababisha wazawa wanaonunua kwao kukosa soko na kuathirika kiuchumi.

"Hoja siyo watu wa Kariakoo kupata maeneo kwenye eneo lile, hoja ni namna gani tunaweza kuwadhibiti Wachina wasifanye biashara za rejareja zinazoweza kufanywa na Watanzania," alisema.

Aliitaka serikali kuongezea fedha wizara hiyo ili ifanye utafiti namna rasilimali zilizopo zinaweza kuongezewa thamani na ili kumudu ushindani katika soko la kimataifa, kwa kuwa kutengemea fedha za wahisani katika utafiti kunawapa maarifa ya kuboresha masoko yao.

Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kirumbe Ng'enda, aliitaka serikali kuweka miundombinu rafiki ya usafirishaji bandarini, ili kuvutia nchi jirani kupitisha mizigo yao na kukuza biashara.

Alisema serikali pia iweke miundombinu rafiki ya uwekezaji ili kuwavutia wafanyabiashara, akitaja maeneo yanayolalamikiwa kuwa ni benki kukosa mifumo rafiki ya kukopesha na TRA kufunga akaunti za wawekezaji.

Alisema wafanyabiashara wakubwa wanapokuja kuwekeza nchini wanalazimika kwenda kwenye taasisi za kifedha za nje ya nchi ili kuwasaidia katika uwekezaji wao.

Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei aliitaka serikali kuwekeza nguvu kwenye kuvitambua na kuvirasimisha viwanda vidogo kwa kuwa vipo vingi mitaani, havilipi kodi na kusababisha kuharibu biashara na serikali kukosa mapato.

Pia aliitaka serikali kufanyia kazi changamoto wanazokabiliana nazo wafanyabishara wazawa ikiwamo TRA kukagua hesabu za miaka ya nyuma licha ya Rais Samia Suluhu Hassan kuweka ukomo.

"Mfano, Rais Samia aliweka ukomo wa TRA kukagua na kutathmini mahesabu ya kampuni ili kuona kama zililipa kodi zao sawasawa, lakini bado wanakwenda wanataka hesabu za miaka mitatu kwa kisingizio cha tathmini," alisema.

Awali akiwasilisha bajeti hiyo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji aliomba Bunge liidhinishe Sh. bilioni 110.9 ili kutekeleza vipaumbele vyake sita ikiwamo kuboresha mazingira ya uwekezaji viwandani na ufanyaji biashara.

Waziri huyo alisema kuwa kwa mwaka ujao wa fedha watafanya intelijensia ya masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini kwenye masoko ya kimkakati na ya kimataifa na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi nchini.

Alisema serikali imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika viwanda vya kuzalisha mafuta vya ndani, ili kupunguza bei ya mafuta ya kula yaweze kushindana na mafuta yanayotoka nje ya nchi.

Alisema viwanda hivyo vinazalisha chini ya uwezo wake kutokana na kukosekana kwa malighafi ya mbegu bora na za kutosha za mafuta.

Aliwahakikishia wawekezaji kuwa serikali iko tayari kuwalinda na kuwasihi waendelee kuleta mitaji na kufanya biashara zao kwa amani.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA. 961 MWAKA 2024**

**AMICUS TANZANIA LIMITED ....................MDAI**

**DHIDI**

1. **SUNLIGHT TOURS**
2. **SUN TRUST CO. LTD..................WADAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: SUN TRUST CO. LTD**

Kwa kuwa mdai aliotajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinazopatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 29/05/2024 saa tatu kamili (09:00) asubuhi mbele ya Mheshimiwa jaji B.K.Philip, kwaajili ya kujibu madai hayo dhidi yako.

**ANGALIA**

Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa ulipokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kutumia katika utetezi wako siku hiyo. Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya mahakama leo tarehe 22 mwez..i 4.. 2024

THE HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha **Nipashe** au **The Guardian** kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende **"pay via mobile"**. Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote **1-6**



Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Kampeni ya madaktari bingwa wa Samia yafikia watu 20,900

**Na Mwandishi wetu**

KAMPENI ya madaktari wa Rais Samia Suluhu Hassan iliyozinduliwa Mei 6, mwaka huu, mkoani Iringa, imetoa huduma katika halmashauri 56 ndani ya mikoa tisa ya Tanzania Bara kwa kuwahudumia wagonjwa 20,922.

Msemaji wa Wizara ya Afya, Englibert Kayombo, akizungumzia kampeni hiyo jana, alisema kati ya wagonjwa hao watoto ni 1,170, ambao walipata huduma mbalimbali.

Kuhusu mafanikio ya kampeni hiyo, alisema mpango huo umeonyesha uhitaji mkubwa wa wagonjwa walioonwa na wataalam wa afya waliokuwapo katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara.

"Kwa sasa madaktari hawa wanatoa huduma katika hospitali za halmashauri. Lengo halisi ni kufika maeneo ya chini kabisa ili kuwasaidia Watanzania wote.

"Serikali inataka kupunguza kama si kuondoa kabisa changamoto za Watanzania, hivyo kupitia program mbalimbali za Wizara ya Afya, tunaamini kwa kiasi kikubwa itasaidia wananchi katika maeneo yote ambayo madaktari hawa watatoa huduma," alisema Kayombo.

Kayombo alisema mbali na kutoa huduma za afya kwa wagonjwa, wataalam hao watatumia ujuzi wao kuwanoa wataalam wa afya katika maeneo watakayopita ili kuwasaidia katika utoaji huduma endelevu.

Mikoa ambayo mpaka sasa madaktari bingwa wa Rais Samia wametoa huduma ni Iringa, Njombe, Songea, Mbeya, Songwe, Lukwa, Manyara, Singida na Dodoma.

Kampeni hiyo ilizinduliwa Mei 6, mwaka huu, mkoani Iringa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ambaye alisema wataalam hao wameangalia maeneo yenye uhitaji mkubwa zaidi kama vile madaktari bingwa wa afya ya uzazi na wanawake, watoto na watoto wachanga.

Wengine ni daktari bingwa wa upasuaji, daktari bingwa wa magonjwa ya ndani na daktari bingwa wa usingizi na ganzi ambao kwa pamoja wanafikia 25 na watatoa huduma kwa siku tano za wiki.

Kwa mujibu wa Kayombo, madaktari hao wiki hii wanatoa huduma Arusha, Kilimanjaro na Tanga, hivyo kuongeza idadi ya mikoa itakayokuwa imenufaika na huduma hiyo ya madaktari bingwa wa Rais Samia.

Madaktari hao wamepiga kambi Muheza mkoani Tanga kwa siku nne na kuleta mafanikio makubwa ikiwamo kuwapunguzia wananchi gharama za kufuata huduma za kibingwa kwenye hospitali kubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah, baada ya kuzindua kampeni hiyo katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza iliyoko Kijiji cha Lusanga, alisema kambi hiyo imeonekana kuwa na tija kwa wananchi kwa kuwa imepunguza gharama za kufuata huduma za kibingwa nje ya wilaya.

Timu hiyo ya madaktari bingwa waliowasili mkoani Tanga wameanza kutoa huduma katika hospitali za wilaya zote mkoani humo huku wito ukitolewa kwa wananchi kujitokeza kupata matibabu ili kupunguza ghalama kwa kufuata huduma hizo katika hospitali kubwa nchini.

Nipashe ilifika katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza na kushuhudia huduma zikiendelea kutolewa kwa wagonjwa wenye matatizo mbalimbali chini ya uangalizi wa madaktari hao bingwa.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk. Juma Mombokaleo, alisema wagonjwa wameendelea kujitokeza katika hospitali hiyo kupata huduma mbalimbali wakiwamo wanawake na wenye changamoto ya uzazi.

**Imeandikwa na Mwandishi Wetu (DAR) na Steven William (MUHEZA)**

# Wanne wa familia moja walazwa baada ya kumwagiwa kemikali

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATU wanne wa familia moja wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kutokana na kuungua moto baada mmoja wao kuwamiminia wenzake kimiminika kilichodhaniwa ni mafuta yenye asili ya mlipuko yaliyosababisha kuunguza nyumba yao iliyoezekwa kwa nyasi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Mei 19 mwaka huu saa mbili usiku katika Kijiji cha Gonja, Kata ya Pemba, wilayani Mvomero.

Mkama alisema kuwa kutokana na tukio hilo, polisi kwa kushirikiana na wadau wengine wa matukio ya moto wanafanya uchunguzi wa tukio hilo linalodaiwa kufanywa na Paschal Paul (18) na kusababisha majereha kwake pamoja na ndugu zake watatu.

Kamanda huyo alisema Paschal inadaiwa aliwakusanya ndugu zake watatu kwa lengo la kuwapasha habari, lakini akawamiminia kimiminika kilichodhaniwa kuwa ni mafuta yenye asili ya mlipuko.

Alisema kitendo hicho kilisababisha kuunguza moto nyumba yao iliyoezekwa kwa nyasi na kupata majeraha makubwa kwake pamoja na ndugu zake watatu na wote wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Kamanda Mkama aliwataja majeruhi wengine wa moto ni Mathias Elias (34), mkulima; Augustino Elias ( 24), mkulima; na Anjela Elias (12), mwanafunzi na wote ni wakazi wa Kijiji cha Gonja, Kata ya Pemba, wilayani Mvomero.

Alisema inadhaniwa mtuhumiwa huyo ana changamoto ya afya ya akili kwa muda mrefu.




Moja ya majengo yakiwa yamewekwa vyuma 'grill' kwenye maeneo yote ya nyumba kitendo ambacho ni hatari endapo itatokea ajali ya moto kwani itakuwa vigumu katika uokoaji, kama ilivyonaswa na kamera yetu katika Mtaa wa Tandamti, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanufaika wa TASAF wapewa mamilioni ruzuku ya uzalishaji

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SHILINGI milioni 392 zimegawiwa kama ruzuku ya uzalishaji kwa walengwa 1,120 wa Mpango wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na kuondoka kwenye mpango kwa hiari katika mitaa 164 ya Manispaa ya Morogoro.

Akizungumza wakati wa ugawaji ruzuku kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Emmanuel Mkongo, Mratibu wa TASAF Manispaa ya Morogoro, Feliciana Katemana alisema jana kuwa walengwa hao wamepatiwa ruzuku hizo ili waanzishe na kuendeleza miradi yao ya kiuchumi.

Katemana alisema Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na TASAF makao makuu ilizijengea uwezo kaya 1,146 za walengwa wanaotekeleza mpango wa TASAF ya awamu ya kwanza kutoka katika mitaa 164 ambazo ni sawa na asilimia 70 ya kaya za mpango huo.

"Kila mlengwa aliyekidhi vigezo amelipwa Sh. 350,000, vigezo ni lazima mlengwa awe na mwalikishi wa kaya ya walengwa wa TASAF, awe na umri kuanzia miaka 18 na si zaidi ya miaka 65 na mwenye uwezo wa kufanya kazi, awe amesimamiwa na wataalamu wa ugani na aweze kuandaa mpango huku akiwa tayari kutoka katika mpango huo kwa hiari akishapokea ruzuku kama ilivyokuwa kwa walengwa hawa," alisema Katemana.

Alisema kuwa tayari walengwa wote walishaandaliwa kisaikolojia na kutambua kuwa wakilipwa ruzuku ya uzalishaji ni sehemu ya kuhitimu katika mpango huo kwa hiari ili wajitegemee kwa kutumia ruzuku hiyo kama mtaji au kuongeza mtaji wake waliokuwa nao.

Alisema wapo walengwa wengine walishaanza biashara kwa kutumia fedha za ruzuku walizokuwa wanapewa mwanzoni na kwamba fedha walizogawiwa sasa watakuza biashara zao na kuinua kipato cha kaya na uchumi ili kuleta maendeleo endelevu na kujitegemea bila msaada.

"Tayari walengwa waliokwishapata ruzuku wamejiunga katika vikundi vya kuweka na kuwekeza na wataalamu wanaendelea kuwajengea uwezo ili pale mikopo ya asilimia 10 ya manispaa itakapoanza kutoka nao wanufaike na fursa hiyo," alisema.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Pascal Kihanga aliwataka walengwa kuzitumia fedha za ruzuku walizopata kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuinua uchumi wao.

Mmoja wa walengwa hao, Watende Selemani alishukuru serikali kupitia TASAF kwa kutuongezea ruzuku hadi Sh. 350,000 kutoka Sh. 48,000 za awali kwa ajili ya kukuza biashara zao.

Selemani anayefanya biashara ya genge hivi sasa, alisema ruzuku hiyo itasaidia kuinua kibiashara na kupiga hatua kiuchumi.

# Makonda kuzuru wilayani kupembua mbivu na mbichi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, ametangaza siku sita za moto atakazotumia kukagua miradi ya maendeleo katika halmashauri zote za mkoani hapa.

Pia amesema katika ziara hiyo, atafanya mikutano ya hadhara kusikiliza kero za wananchi.

Makonda alisema hayo jana wakati akikabidhi magari mawili kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Arusha, yaliyotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

"Tutakuwa na siku sita za moto kwenye mkoa wetu kuanzia Mei 23 mpaka 30, mwaka huu. Tutakwenda kwenye halmashauri zote kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na serikali,pamoja na kuzungumza na wananchi kupitia mikutano ya hadhara," alisema.

Makonda pia alitoa angalizo kwa watumishi wa serikali kuanzia ngazi za vijiji, mitaa na halmashauri ambao watabainika kuwa wameshindwa kusimamia miradi ya maendeleo na jambo linalohusu wananchi moto utawawakia.

"Mtendaji yeyote kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji, mtaa na halmashauri kama kuna mradi umeshindwa kusimamia au jambo linalohusu wananchi halijafanyika vizuri, moto utakuwakia nyumbani kwako na moto huu hautakuwa na huruma.

"Nimeshazungumza na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha (RMO), wakati wa ziara hiyo, kama kuna mtumishi atazidiwa kutakuwapo na watoa huduma ya kwanza kwa ndege na atatibiwa na baadaye atarudi kuja kujibu tuhuma za wananchi.

Hata hivyo, alisema kama kuna mtumishi wa serikali amekwenda mkoani humo kwa kuandikiwa kimemo kwa nguvu ya mtu fulani aliyempeleka kufanya kazi katika eneo hilo wote watang'oka kwa kuwa hawatakuwa na nguvu.

"Kama kuna mtumishi uko katika mkoa huu,kwa kuandikiwa kimemo ukitegemea nguvu ya mtu fulani aliyekuleta hapa nakwambia wewe na huyo mtu wako mtang'oka au utanyooka ili kulinda heshima ya kiti hiki.

"Tunataka uwajibikaji iwe nguzo kwa watumishi wa serikali,pia ninaomba wananchi wa Arusha, pale mnapojua kuna haki zenu msisite kusema kwa ujasiri kwa kuwa tunataka haki iwe msingi wa maendeleo ya mkoa wetu.alisema Makonda.



Muuguzi kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Patrice Justine (kushoto), akimpima shinikizo la damu, Shani Said, wakati wa kambi ya siku mbili ya huduma ya upimaji wa magonjwa ya moyo bure katika Taasisi ya JKCI Dar Group, kuadhimisha Siku ya Shinikizo la Juu la Damu, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Prof. Mukandala: MV Bukoba ilikuwa 'bomu' tangu ununuzi

**Christina Mwakangale na Vitus Audaux**

JANA ilitimu miaka 28 kamili tangu kuzama kwa meli ya Mv Bukoba' katika Ziwa Victoria, Profesa Rwekaza Mukandala akiibua hoja mpya ikiwamo miili ya abiria kuelea kwa muda mfupi kwenye maji kunakotoa ishara walikunywa mafuta kabla ya kufariki dunia.

Vilevile, msomi huyo amesema meli hiyo ilizama kutokana na uzembe, haikusajiliwa licha ya kufanya kazi kwa miaka 17 huku nahodha wa meli hiyo akijiokoa kwanza na kutelekeza abiria wake.

Prof. Mukandala aliyasema hayo jana, mkoani Dar es Salaam, katika Mhadhara wa Uprofesa uliofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na kuhudhuriwa na wanazuoni pamoja na Mkuu wa chuo hicho, Rais mstaafu Jakaya Kikwete.

Akiwasilisha mada kwa takribani saa moja na nusu, Prof. Mukandala alisema: "Tume ya Jaji Kisanga ilitaja upungufu ya meli. Kati yake, ni meli kuongozwa na manahodha wasio na ujuzi, kujaza mzigo hasa ndizi na abiria zaidi ya 400, mara mbili ya kiwango kilichostahili."

Prof. Mukandala alisema Taasisi ya Maji ya Dermark iliwahi kufanya utafiti na kushauri meli hiyo iwe na matangi yaliyojaa maji muda wote ili kuweka uwiano wenye usawa kutokana na kasoro za meli tangu ilipoundwa na wahandisi wasio na ujuzi.

"Mnusurika maarufu anapinga maelezo kuhusu ubovu wa chombo. Rushwa na uendeshaji duni wa chombo, kutofanyiwa matengenezo kulichangia meli kuzama. Meli hii ilikuwa ikitembea upande na ikisererekа majini," alisema mwanazuoni huyo.

Prof. Mukandala alieleza kuwa inaaminika kwamba binadamu akizama huibuka baada ya siku kadhaa. Lakini mnusurika mmoja alisema wakati anajiokoa alizingirwa na mikungu ya ndizi na miili ya watu. Inawezekana walipigwa na shoti ya umeme au walikunywa mafuta.

Alisema pamoja na tukio hilo kutokea, likiwa ni miongoni mwa yaliyo makubwa nchini na kimataifa, baada ya miaka 15, ajali nyingine ya meli ikatokea, Mv Islander ikazama Bahari ya Hindi na kupoteza maisha ya takribani watu 1,000.

Prof. Mukandala alisema meli hiyo ilianza kazi mwaka 1979, ikiwa na kasoro kadhaa ambazo zilifanya isisajiliwe, akiutaja ubeberu kuwa chanzo cha meli kuzama.

"Serikali iliamua kutumia mkopo kununua meli kutoka Serikali ya Ubelgiji iliyoikopesha faranga za Kibelgiji milioni 500 wenye riba ya asilimia 8.3 kwa kipindi cha miaka saba.

"Ununuzi mzuri wa huduma ni ule wa kutangaza kwa ushindani, serikali haikufuata mchakato wa ununuzi uliozoeleka na mkopo ulikuwa wa pingu wenye masharti magumu sana.

"Serikali ya Ubelgiji iliteua kampuni ya ununuzi, kampuni ya MS Belgium Shipping ilikuwa ni kati ya muungano wa kampuni tatu zilizopata zabuni hiyo. Shirika la Reli (msimamizi wa wakati huo) lilieleza aina ya meli inayohitajika," alisema.

Profesa Mukandala alisema kuwa meli hiyo licha ya kufanyiwa majaribio kadhaa, ilibaki kazini ikiwa na kasoro ingawa hakuna hatua zilizochukuliwa, hivyo kuhatarisha uhai wa wasafiri.

Alisema Shirika la Reli Tanzania halikuwa na muda wa kupitia na kusoma vifungu vya mkataba wa ununuzi. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wakati huo aliagiza mkataba utiwe saini haraka.

"Inaonesha naye waziri alipewa maagizo na Rais ambaye ana madaraka makubwa, akisema linatekelezwa. Tume ya Jaji Kisanga ilisema masharti yalikuwa magumu sana," alisema.

Prof. Mukandala alisema ujenzi wa meli wa meli ulifanyika Tanzania na watu 63 ambao tume ilibaini hawakuwa na ujuzi chini ya msimamizi mmoja kutoka Ubelgiji.

Alisema kuwa Julai 27, 1979, meli ilikabidhiwa kwa Rais Julius Nyerere na kuanza kazi mwezi uliofuata. Mamlaka zote tatu; dola, Shirika la Reli hazikuchukua hatua baada ya meli kubaini kuwa na kasoro.

"Ili kukabiliana na kasoro hizo, ilibidi ibebe maji katika matangi muda wote. Uokoaji ulikuwa na kasoro wakati ajali ilipotokea. Hakukuwa na mtaalamu wa uzamiaji hata mmoja, maboya 'kiduchu' licha ya meli kuchukua takriban saa nne. Meli ya Titanic ilizama ndani ya saa tatu lakini watu wengi waliokolewa," alisema.

Prof. Mukandala alisema, "tunajifunza kwamba madaraka ya Rais ni makubwa, kuna haja ya kuwa na mjadala kuwapo Katiba Mpya. Rais Nyerere aliruhusu hili, meli inunuliwe.

"Kuna wakati meli ilijaa maji na kuelemea upande mmoja, lilitolewa tangazo la ununuzi ili kuepusha rushwa katika mchakato wa mradi wowote."

Kukiwa na hoja hizo za Prof. Mukandala, wananchi kutoka mikoa ya Kagera na Mwanza wamelalamikia serikali kutoipa hadhi siku ya kumbukumbu ya ajali hiyo.

Mmoja wa wananchi hao, Juma Rutaiwa kutoka mkoani Kagera, alisema jana kuwa licha ya tukio hilo kuwa kubwa katika kumbukumbu za Watanzania, historia yake ipo hatarini kupotea kutokana na kutokupewa kipaumbele kama yalivyo matukio mengine ya kihistoria.

"Awali lilikuwa na hamasa kubwa tunafanya ibada ya pamoja tukiwa wengi kwa ushirikiano na serikali pamoja na kampuni ya meli lakini kwa sasa hali ni tofauti, ni sisi wachache pamoja na baadhi ya viongozi wa dini,"alisema Rutaiwa.

Mfanyausafi katika makaburi ya MV Bukoba, Mussa Ntobi alisema usalama katika makaburi hayo upo vizuri licha ya kuvamiwa na mafuriko ya mvua yaliyosababisha jukwaa la kumbukumbu kubomoka na makaburi hayo kuvamiwa na maji.

Paroko wa Parokia ya Nyamongoro, Padre George Nzungu ambaye alishiriki katika sala fupi ya kumbukizi katika makaburi jana, alisema ajali hiyo ilitokea akiwa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mwanza.

Kampuni ya Huduma za Meli Nchini (MSCL) imewahakikishia Watanzania kuwa itaendelea kusimamia ipasavyo usafiri pamoja na udhibiti wa vyombo vya majini ili kuhakikisha vinatoa huduma bora.

Meli ya MV.Bukoba ilipata ajali Mei 21, 1996 mwambao wa Bwir, jijini Mwanza ikiwa na abiria kati ya 750 na 800 pamoja na wafanyakazi 37 zikiwa zimesalia kilomita 48 kufika nchi kavu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukosefu madawati shuleni ni jambo ambalo halikubaliki

**MOJA** ya taarifa zilizojitokeza kwenye vyombo vya habari jana ni juu ya kubainika kuwa kuna shule mojawapo katika Manispaa ya Singida, inakabiliwa na uhaba wa madawati hatua ambayo imesababisha wanafunzi 486 kukaa sakafuni wakati wa masomo.

Shule hiyo ya msingi ambayo ilianzishwa mwaka 2013 ikiwa na wanafunzi 63 inakabiliwa na uhaba wa madawati 162 kwa sababu ya ongezeko la wanafunzi ambao kwa sasa wamefikia 1,182. Katika maelezo yake kwa wajumbe wa kamati ya shule, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Hedwiga Mtalo, alisema tatizo hilo ni la muda mrefu.

Kwa mujibu wa mwalimu mkuu huyo, tatizo hilo la madawati lingekuwa limeshatatuliwa muda mrefu lakini mwitikio hasi wa wazazi ndio umesababisha kuendelea mpaka sasa. Wazazi hao walitupiwa mzigo wa lawama kwamba wameshindwa kutekeleza makubaliano waliyojiwekea kuhusu kutatua jambo hilo.

Licha ya mwalimu huyo kusema hivyo, Diwani wa Misuna, Hamisi Kisuke, naye alijitetea kwamba ana mzigo mkubwa katika kusimamia maendeleo ya kata ikiwamo kumaliza changamoto zilizoko ndani ya eneo hilo, hatua iliyomfanya mwenyekiti wa kamati ya shule kuomba serikali kuingilia kati tatizo hilo kwa kupeleka madawati.

Hata hivyo, Ofisa Elimu Msingi wa Manispaa ya Singida, Omari Maje, aliyekuwapo katika msafara wa kamati hiyo, kuna makubaliano na wazazi kwamba kila mmoja achangie Sh. 6,000 ili kununua madawati 81 ya kuanzia ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha elimu.

Suala la wanafunzi katika shule hiyo kukaa sakafuni kwa sababu ya ukosefu wa madawati limeibua hoja nyingi kwa kuzingatia kuwa iko ndani ya Manispaa. Moja ya hoja ni kwamba iwaje kuwapo kwa tatizo hilo ilihali eneo ilipo ni makao makuu ya mkoa ambako viongozi wengi wa mkoa na wilaya wako karibu na shule.

Kwa miaka kadhaa, serikali katika ngazi za mikoa na wilaya imekuwa ikisisitiza ujenzi wa miundombinu ya elimu pamoja na samani yakiwamo madawati. Sasa iweje shule hii iliyoko katika eneo la mji isahaulike katika hilo? Viongozi walikuwa hawalijui tatizo hilo hadi inabainika sasa kuwa shule ina uhaba wa madawati?

Jambo hili linapaswa kuwaamsha viongozi katika sehemu mbalimbali kwa kuwa inawezekana shule hiyo ni mfano tu wa nyingi zinazokabiliwa na matatizo lakini viongozi hawasemi kweli ama kwa kuhofia kuchukuliwa hatua au kulazimishwa kuwajibika. Haiwezekani kila mwaka serikali ihimize kumalizwa kwa matatizo katika sekta ya elimu, likiwamo la madawati, yanayosababishwa na ongezeko la wanafunzi kila mwaka halafu baadhi ya viongozi katika maeneo kushindwa kutekeleza.

Ni wakati mwafaka sasa kwa serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na sekretarieti za mikoa kufanya ukaguzi katika shule mbalimbali ili kubaini matatizo yanayozikabili shule nchini.

Ni dhahiri kwamba mambo mengi yaliyojificha yatawekwa bayana ili yapatiwe ufumbuzi badala ya viongozi wanaopaswa kutekeleza majukumu hayo kunyamaza na kuacha matatizo kuendelea. Yako matatizo mengi katika shule nchini lakini watendaji, kwa sababu ya uoga, wanakaa kimya.


Gazeti hili liliwahi kufichua matatizo yanayoikabili shule moja katika wilaya ya Mpwapwa na katika hatua ya awali, viongozi wa mkoa na serikali kuu ikiwamo TAMISEMI, waliibuka na kusema ni uzishi lakini walipokwenda walibaini kuwa kilichoandikwa ni ukweli mtupu na hatimaye nguvu zikaelekezwa na sasa tatizo limetatuliwa.

Kwa mantiki hiyo, ni vyema ukaguzi ukafanywa kila wilaya na halmashauri nchini ili kuainisha changamoto inazozikabili zikiwamo madawati, majengo hatarishi kwa wanafunzi na walimu na uhaba wa matundu ya vyoo na hatimaye kuchukua hatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Mwandishi Wetu

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwisho wa muhula umefuatilia wanao

**SHULE** zinakaribia kufungwa na sasa watoto wako kwenye maandalizi ya mitihani au wengine wameshaanza. Wazazi na walezi ni wakati wa kujihoji tumefuatilia elimu ya watoto wetu kuanzia Januari hadi sasa?

Ukweli ni kwamba karibu kila kona ya Tanzania kumekuwa na tabia ya wazazi au walezi kulipa gharama za elimu ya watoto wao bila kufanya tathmini na ufuatiliaji katika elimu ya wanafunzi hao wa ngazi mbalimbali.

Wanaamini kuwa jukumu la kufanikisha elimu ya watoto wao linaishia katika kulipa ada na michango na mahitaji ya shule pekee.

Kama wewe ni mmojawapo jiulize hivi jukumu lako kweli halivuki mpaka huo? Huangalii hata kama anajua kusoma au kuandika kwa ufasaha?

Ikumbukwe kuwa hali hii inasababisha kushuka viwango vya elimu na pia kujiaminisha kuwa wazazi, walezi na familia kujiweka pembeni na kuona kuwa jukumu la kufuatilia maendeleo ya darasani na nidhamu ya watoto wao ni kazi ya walimu shuleni.

Aidha, hali hii ni matokeo ya kuenea kwa utandawazi hasa katika matumizi ya mitandao na kubadilika kwa mifumo ya maisha ikiwa ni pamoja na wazazi na walezi kuwa na majukumu mengi ya kutafuta pesa na mahitaji mengine ya kulinda familia.

Mambo hayo husababisha wazazi au walezi kukosa muda wa kufanya ufuatiliaji wa maendeleo ya elimu ya watoto wao ikiwa ni pamoja na kukosa muda wa kuongea na watoto wao juu ya changamoto zao za kielimu.

Tatizo liko kwa waajiriwa, waliojiajiri na wafanyabiashara na kila mmoja ambaye ni mlezi au mzazi wanasaka kipato na kutafuta hela hivyo huondoka nyumbani alfajiri na mapema na kurudi baada ya saa 4:00 usiku na kukuta watoto wameshalala.

Baadhi ya walezi na walezi wametingwa na vikao vya kila aina vya ofisini, sherehe za kifamilia kuanzia harusi, sikukuu za kuzaliwa na hata masuala ya kiimani na kusababisha kukosa muda au kutumia saa chache kukaa na watoto wao na kushindwa kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kutambua maendeleo na changamoto za kielimu za watoto wao.

Hata sasa muhula unapokwisha wazazi na walezi wanaendelea kujisahau na kujiaminisha kuwa wanalipa ada na watoto wanasoma shule wanazoziamini kuwa ni za viwango, wanagharamia usafiri na nyumbani kuna kila huduma kuanzia chakula na burudani.

Wanawapatia televisheni ili kuangalia katuni, wanawapatia vishkwambi kucheza michezo na kujivinjari na vikaragosi lakini yote hayo wanajisahau kuwa mwisho wa haya yote ni madhara kwenye elimu ya watoto wao ikiwa ni pamoja na kutofuata ratiba za masomo na kushindwa kuhudhuria shuleni kikamilifu.

Ukweli ni kwamba watoto wao wanakosa uangalizi wanaondoka nyumbani na kushinda mtaani kwenye michezo ya kompyuta na kutazama video na tamthilia kwenye vibanda umiza na hata kuingia kwenye uhalifu.

Wakumbuke kuwa chanzo kikubwa cha yote haya ni kutokuwapo kwa tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa wazazi au walezi kwenye elimu ya watoto wao hivyo kushindwa kujua na changamoto za kielimu za watoto wao na nini kifanyike kuwafikisha kwenye elimu bora.

Walezi na wazazi wakumbuke kuwa kushindwa kuchukua hatua stahiki za kutatua changamoto za kielimu zinazowakabili watoto wao kunachangia wasijue kusoma wala kuandika yakiwamo majina yao.

Tunapomaliza muhula wazazi kumbukeni kuwa kufuatilia kwa ukaribu ni muhimu sana katika kila kitu ambacho mmewekeza rasilimali, juhudi na nguvu, hivyo kuweni karibu katika masuala ya elimu ya watoto kwani mmewekeza hela, nguvu, hisia na muda wenu.

Kuanzia sasa fahamuni kuwa hili ni jukumu muhimu la wazazi na walezi kwa watoto wao na sio kulipa gharama za masomo pekee, tengeni muda kila wakati iwe jioni, mwisho wa wiki au lolote mtakalopanga licha ya kuwa na shughuli nyingi ili kuwahudumia.

Waulizeni nini anachosoma, kinachomsumbua ikiwa ni pamoja na kupitia na kukagua daftari za watoto ili kuona kilichoandikwa pamoja na tarehe ya somo, mazoezi waliyopewa na amefanya mangapi na kwa kiasi gani na mangapi hajafanya na kwanini hakufanya?

Watafuteni walimu wa masomo mbalimbali na walimu wa madarasa kujua wapi wanatatizika na vipi watapata ufumbuzi kwa kushirikiana.

## Ukaguzi wa kushtukiza kunasa wanaochezea vipimo

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo (WMA) utaendelea na operesheni zake za kushtukiza kwenye maeneo mbalimbali ili kunasa wafanyabiashara wanaochezea vipimo.

Jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa WMA Mkoa wa Ilala, Muhono Nashon, alitangaza hatua hiyo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani iliyofanyika kwenye Soko la Ilala.

Alisema vipimo vingi vinatumika kwenye maeneo ya masoko na ndiyo sababu WMA imeamua kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa Soko la Ilala, baadhi ya vikundi vilipewa mizani bila malipo kama motisha ya kutumia mizani iliyohakikiwa.

"Wale wanaochezea vipimo tunawasihi waache kwa sababu sheria ya sasa ni kali na adhabu imeongezwa, tunawasihi wahakikishe mizani yao imehakikiwa kwa kuweka stika kutoka WMA.

"Kosa moja la kuchezea mzani linaanzia faini ya Sh. 100,000 hadi milioni 20, hivyo mfanyabiashara akitozwa faini kama hii ni dhahiri atayumba kimtaji," alisema.

Nashon alisema uelewa kuhusu vipimo sahihi umeongezeka kwa kiwango kikubwa na wafanyabiashara wengi wameanza kutumia mizani zilizohakikiwa na wakala.

"Tunapotoa elimu hii tunataka watu wote waache kutumia vipimo vya kienyeji, watumie vipimo sahihi na vilivyohakikiwa na tunapofanya msako na kukuta watu wanatumia vipimo batili tumekuwa tukitoa adhabu kali. Kwahiyo, wafanyabiashara wasisubiri tufanye msako, wanapaswa kutii sheria," alisema.

Nashon alisema chimbuko la maadhimisho ya Siku ya Vipimo ni mataifa 17 yaliyokutana mwaka 1875 yakaamua kutia saini mkataba wa haki vipimo ili kuwe na vipimo sahihi kote duniani.

"Lengo la haya mataifa lilikuwa ni kuweka viwango vya vipimo duniani, kwamba ukienda nchi fulani unakuta vipimo vinavyotumika ni vilevile vinavyotumika katika nchi mbalimbali," alisema.

Mwenyekiti wa Soko la Ilala, Ali Mbiku alipongeza WMA kwa uamuzi wake wa kuwapa elimu wafanyabiashara wa soko lake ili watumie vipimo vilivyohakikiwa.

"Mimi binafsi nitaendelea kutoa hamasa kwa wafanyabiashara wa soko hili ili ufike wakati kila mmoja kwenye soko hili awe na mizani iliyohakikiwa na wakala ili mnunuzi apate kiwango cha bidhaa kinacholingana na thamani ya fedha alizotoa," alisema.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala, Charangwa Selemani, aliwataka wafanyabiashara kuacha kucheza na vipimo kwa kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa watakaobainika.

Charangwa alisema kuwa kwa muda mrefu, serikali imekuwa inahimiza matumizi ya vipimo sahihi kwa wafanyabiashara kwa kutumia mizani yenye nembo ya WMA na ambayo ni sahihi.

"Wafanyabiashara kwenye masoko wamezoea kutumia vipimo vya kienyeji, hivyo tumeanza kutoa elimu na kuwapa motisha ya mizani mitano iliyohakikiwa na WMA kwa vikundi vitano vya wafanyabiashara," alisema.

"Tunatoa wito kwa wafanyabiashara wote kuacha kutumia lumbesa na waache kuchezea vipimo. Wananchi ombeni kupimiwa bidhaa kwa vipimo rasmi kwa sababu hivi vya kienyeji wakati mwingine mnapunjwa," alisema.

Alipongeza WMA kwa kutoa elimu mara kwa mara kwa wafanyabiashara. Inawajengea uelewa kuhusu umuhimu wa matumizi sahihi ya vipimo ili keupuka faini.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala, Charangwa Selemani (katikati), akikabidhi mzani kwa mmoja wa viongozi wa vikundi vya wafanyabiashara wa soko la Ilala, jijini Dar es Salaam jana. Wa (pili kushoto) ni Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Ilala, Muhono Nashon. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mikoa yenye mbwa wengi zaidi hii hapa



## Serikali yakosolewa kutumia risasi kuwaua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIKOA ya Geita, Mwanza na Tabora inaongoza nchini kwa kuwa na mbwa wengi kwa mujibu wa taarifa ya Sampuli ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2020.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Yustina Rahhi aliyetaka kujua idadi ya mbwa nchini.

Mnyeti alisema kuna mbwa 2,776,918 nchini na mikoa iliyoongoza kwa mbwa wengi ni Geita (302,879), Mwanza (287,270) na Tabora (243,768).

Alisema wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika kuhakikisha takwimu sahihi za mifugo ikiwamo mbwa zinapatikana kwa wakati ili kuwezesha mipango ya serikali ya kuendeleza sekta ya mifugo.

Akiuliza swali la nyongeza, mbunge huyo alisema ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni changamoto kubwa hasa kwa jamii ya wafugaji walioko vijijini na matibabu yake ni shida kwa sababu hayapatikani katika zahanati na vituo vya afya, hivyo takribani Watanzania 1,500 hupoteza maisha kila mwaka.

"Serikali ina mpango gani kudhibiti kichaa cha mbwa nchini? Njia pekee ambayo serikali inatumia kudhibiti mbwa wazururaji ni kuwapiga risasi. Kwanini serikali inakiuka haki za wanyama?" alihoji.

Pia alitaka serikali kufikiria kufanya alichokiita uchumi wa mbwa kutokana na idadi kubwa ya mbwa nchini kwa kuwafundisha na kuwauza ndani na nje ya nchi.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Mnyeti alisema serikali imeshatoa rukhsa wadau mbalimbali kutoa chanjo kupitia sekta binafsi ili kukabiliana na kichaa cha mbwa.

"Dawa ya kwanza ya kichaa cha mbwa ni kumchanja mbwa mwenyewe, tusisubiri mpaka mbwa augue kichaa cha mbwa ndipo achanjwe, kwa sababu anapougua matibabu yake huwa ni muhimu sana.

"Nitoe rai kwa wadau wote kuendelea kuchanja mbwa ili kudhibiti kichaa cha mbwa kwa sababu hakuna mbadala mwingine tofauti na hapo," alisema.

Mnyeti alisema mkakati wa serikali ni kuhakikisha mbwa wote ambao wamo ndani ya nchi wanaendelea kuchanjwa kwa wakati.

Kuhusu mkakati wa kuzuia mbwa wanaozurura mitaani, Mnyeti alisema mbwa anapokuwa ameshaumwa kichaa kumdhibiti ni pamoja na kuchukua hatua ngumu ya kumuua.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Hali ilivyo katika Mtaa wa Mabibo Mgundini, Kata ya Mabibo wilayani Ubungo, Dar es Salaam. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Maisha mapya ya wenyeji mto ukivamia makazi yao

**Na Halfani Chusi**

ATHARI za mabadiliko ya tabianchi hivi sasa zinaonekana dhahiri. Angalia maisha mapya ya wakazi wa Mabibo Mgundini, wilayani Ubungo, Dar es Salaam:

Mto Gide umefuata makazi yao, nyumba 13 zimebomolewa na maji ya mto huo; kati ya nyumba 1,000 zilizonusurika, baadhi 'zinaning'inia mtoni'; mvua ikianza kunyesha, wakazi wanalazimika kutoka katika nyumba zao kama tahadhari ya kuepusha maafa.

Mwajuma Athumani ni mkazi wa eneo hilo. Nyumba yake imebomolewa na maji ya mto, hivi sasa amejiegesha kwa jirani, akiomba serikali iharakishe ujenzi wa kingo kwenye mto huo kwa kuwa hali inazidi kuwa mbaya.

Anasema zamani kulikuwa na mfereji mdogo ambao hata mtoto wa umri wa miaka minne alikuwa anavuka kwenda upande wa pili, lakini sasa mfereji umegeuka mto mkubwa unaosababisha madhara kwa makazi yao.

"Nipo hapa kwa miaka 50 sasa, kila mwaka mto huu unasogelea makazi yetu, hatimaye hali imekuwa mbaya sana, Mwajuma anasema. Mwaka juzi (2022) na mwaka jana (2023) nyumba tatu zimebomolewa na mto huu.

Serikali itujengee kingo kama ilivyofanya kwenye Mto Ng'ombe, ule wa Sinza (Kinondoni) na kama wataona bora kutuhamisha hapa tupo tayari, lakini watupe fedha ili tuweze kwenda kujenga sehemu nyingine kwa sababu maji haya yametufuata. Zamani hapakuwa na mto hapa, palikuwa na mfereji.

"Tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassani alisikie hili, atusaidie tujengewe kingo. Ninadhani hiyo itakuwa suluhu kwa wakazi wa eneo hili, tutaishi kwa amani na tutakuwa huru kufanya shughuli za uzalishaji kwa maslahi mapana ya taifa letu."

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Harubu Mohamed anasema kama serikali itachelewa kujenga kingo kwenye mto huo, mto huo utapanuka zaidi, hata kuifikia Stendi ya Mabibo.

Mohamed anaungana na Mwajuma kwamba mto huo umebomoa nyumba; yeye ameshuhudia nyumba 13 zikibomolewa na mto huo, Mwajuma akishuhudia nyumba tatu.

"Tayari wenzetu wengine wameezua mabati kwa sababu kilichopo, maji yakijaa mto unafurika hadi kwenye makazi yetu, ndiyo maana unaona nyumba hizi zinaning'inia mtoni, hatuna namna," analalama.

Rajabu Ng'ula ni mkazi wa eneo hilo anayejitambulisha ni mstaafu jeshini. Anasema mto huo hali ilianza kuwa mbaya zaidi miaka mitatu iliyopita kutokana na mto kupanuka zaidi, akisisitiza kujengwa kingo za mto.

Anasema eneo hilo hivi si salama kwa makazi, hivyo kuna haja serikali iwapatie eneo lingine ili wahame.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Said Kitogo, nyumba 1,000 katika mtaa wake ziko hatarini kusombwa na maji ya mto huo.

Mwenyekiti huyo anasema wananchi wanaishi katika eneo hilo kwa mujibu wa sheria. Mto ndio umewafuata.

"Hata Mbunge wa Jimbo la Ubungo (Prof. Kitila Mkumbo) analijua hili na alimtuma katibu wake na wasaidizi siku chache zilizopita walikuja kutoa msaada wa chakula na mahitaji madogo madogo kwa waathirika.

"Lakini ukiangalia lile eneo, nyumba nyingi zipo hatarini. Mto Gide unaanzia Kigogo, unapandisha mpaka Kimara. Madiwani watatu wapo katika mchakato kuitaka serikali ichukue hatua kunusuru wananchi," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema kinachoendelea ni vikao vya mara kwa mara juu ya ujenzi wa kingo ili kunusuru kaya zilizoathirika.

"Serikali ingeanza kuunyoosha kwanza ule mto ili maji yafuate mkondo wake wa zamani. Mto huu ulianza kufuata makazi ya watu miaka 15 na kila mwaka tulikuwa tunausafisha," anasema.

Mwenyekiti huyo anaeleza kuwa pamoja na mabadiliko ya tabianchi kusababisha mvua kubwa, tabia ya utupaji taka mtoni imechangia mto huo kupanuka na kusababisha madhara kwa wakazi wa eneo hilo.

Diwani wa Mabibo, Thomas Klerru, anaungana na Mwenyekiti Kitogo kwamba uchafuzi wa vyanzo vya maji ni miongoni mwa yaliyochangia mto huo kupanuka.

Klerru anasema madhara hayako Kata ya Mabibo pekee, bali pia Kata za Mbezi, Saranga, Kimara, Ubungo, Makuburi, Mabibo, Mburahati, Kigogo na Mkwajuni.

"Muda wowote kazi ya kujenga kingo itaanza. Kinachosubiriwa ni mvua ipungue, kuna uwezekano wa kuhamisha Mto Gide pale Ubungo External, kuchepushia Mto Msimbazi.

"Zamani hatukuwa na mto huo. Nilihamia hapa Mabibo miaka ya 1990, zamani tulikuwa tunapita hapa, hapakuwa na chochote, hata magari yalikuwa yanapita.

"Ulianza kama mfereji, mwisho wa siku umekuwa mto mkubwa kabisa kutokana na kujaa mchanga," alisema diwani huyo.

Mbunge wa Ubungo, Prof. Mkumbo anathibitisha kuwa na taarifa juu ya yanayowakumba wapigakura wake, akieleza kuwa mito mingi Dar es Salaam inazidi kutanuka.

"Si Mto Gide pekee unaosumbua wananchi, ipo mingi kama Mto China, kilichopo ni kwamba tutajenga kingo kwa baadhi ya maeneo yenye changamoto kubwa zaidi.

"Kuna mradi mkubwa unaojenga Bonde la Mto Msimbazi, moja ya maeneo ambayo yataangaziwa katika utekelezaji mradi huo ni Mto Gide na China. "anasema Prof. Mkumbo ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji.

Anataja hatua za awali alizochukua ni pamoja na kutembelea wananchi walioathirika na kuwapa misaada mbalimbali na kujadiliana nao kuangalia namna ya kutatua tatizo hilo, hoja kuu ikiwa kuwashawishi kuhama kabla hawajapata madhara makubwa zaidi.

Hata hivyo, mwandishi alipohoji juu ya fidia kwa wananchi wanaodai mto umewafuata, Prof. Mkumbo alisema, "kwa kweli hilo mimi ni kiongozi, nisiwe muongo, Kwa kawaida serikali huwa inalipa fidia pale ambapo inamwondoa mwananchi kwenye eneo lake kwa ajili ya kupisha shughuli za kiserikali.

"Kwa hili la mto si kwamba serikali inataka kuwaondoa pale, bali inataka kuwasaidia wananchi kujenga kingo kupunguza athari, siwezi kusema wale waliokumbwa watalipwa, hapana!

"Kwa tukio la pale huwezi kuilaumu serikali wala kumlaumu mwananchi, imetokea tu maji yamebadili mwelekeo yamefuata makazi ya watu kutokana na mabadiliko ya tabianchi."

Mbunge huyo anasema kuwa hivi sasa kuna timu ya wataalamu imeundwa na serikali ifanye utafiti mpana kuhusu hali ya mito ya Dar es Salaam na kushauri hatua za kuchukua ili kutatua tatizo.

Jofrey Mkinga, Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Dar es Salaam, anasema madhara yanayoripotiwa Mabibo yameshafikishwa mezani kwake pamoja na hoja ya ujenzi wa kingo za Mto Gide.

Anasema ujenzi wa kingo za mto huo utatekelezwa kupitia Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

"Tumeona namna mto ulivyoharibu makazi ya watu, ni jambo linalofahamika kwa viongozi wote wa Ubungo. Mradi wa ujenzi wa kingo umeshapitishwa. Tutaanza na hatua za usanifu, tutatangaza zabuni za kupata wahandisi washauri ili waingie kazini mapema.

"Viongozi wote wameliona hilo tatizo, kila linapokuja suala la maboresho wanazungumzia Mto Gide, kuujenga mto huo si fedha kidogo, wananchi wawe wavumilivu, serikali imeshaliona tatizo hilo, anasema Mkinga.

Hata hivyo, meneja huyo anakemea tabia baadhi ya watu kujenga bondeni kwa kuwa maji hufuata mkondo, hivyo wazingatie ushauri wataalamu na maelekezo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004), ambayo pamoja na mambo mengine, inazuia kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka chanzo cha maji.

Mtaalamu Mbobezi wa Jiolojia, Dk. Peter Kafumu, anasema silaha ya kwanza kukabili matatizo kama hayo ya Mabibo ni kuzingatia hatua zote za tahadhari zinazowasilishwa na mamlaka husika kitaifa na kimataifa.

Anafafanua kwamba kinachojiri Mto Gide na kwingineko Afrika Mashariki, ni matokeo ya ongezeko la joto juu ya wastani katika eneo la kati la Bahari ya Pasifiki.

Kijiografia bahari hiyo iko kati ya Amerika upande wa mashariki na Bara la Asia/ Australia upande wa magharibi. Ina ukubwa wa kilometa za mraba milioni 179.7 ambazo si tu ni bahari kubwa, bali pia ni eneo kubwa kuliko nchi kavu yote duniani; ni karibu nusu ya uso wa dunia.

Dk. Kafumu anasema panapokuwapo ongezeko la joto kwenye bahari hiyo, athari zake kijiolojia huangukia zaidi Ukanda wa Afrika Mashariki na kwingineko jirani. Ni sehemu ya sababu zinazozua balaa la mvua kubwa nchini na kwingineko Afrika Mashariki.



## Serikali yashinda mashauri 15, yaokoa tril.1.5/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKILI Mkuu wa Serikali, Dk.Boniphace Luhende amesema ofisi hiyo imeokoa Sh.trilioni 1.5 baada ya kushinda mashauri 15 ya usuluhishi kati ya 19 yaliyokuwa yamefunguliwa ndani na nje ya nchi, katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu.

Amesema kati ya mashauri ya madai 7,813 yaliyoendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuanzia Julai 2023 hadi Aprili 2024, mashauri 762 yalimalizika, ambapo mashauri 743 yenye thamani ya Sh.bilioni 406.4 yalimalizika kwa serikali kupata ushindi.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa mafunzo ya siku tatu ya mawakili wa serikali yaliyokuwa na kaulimbiu isemayo 'Uendeshaji wa mashauri ya serikali wajibu wa majukumu ya mawakili wa serikali' yaliyoenda sanjari na uzinduzi wa nembo itakayotumiwa na mawakili wa serikali.

"Licha ya mashauri hayo pia serikali imeendesha mashauri yasiyohusu fedha yenye umuhimu mkubwa kwa ustawi wa taifa letu ikiwemo shauri la mradi wa mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda mpaka Chongoleani-Tanga.

Pia, alisema ofisi hiyo imeshinda shauri la kupinga mkataba wa uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam na shauri la kupinga uwekezaji katika kiwanda cha Saruji Tanga.

Alisema mafunzo hayo yamejikita kwenye maeneo ambayo huzalisha mashauri mengi dhidi ya serikali, ambapo kufikia Aprili 2024 ofisi hiyo iliendesha mashauri 7,813 kati ya mashauri hayo 7,798 yalikuwa ya ndani ya nchi na mashauri 15 yalikuwa nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Dk.Luhende, ofisi hiho iliendesha mashauri mengine 179 kwa kipindi hicho, ambapo mashauri 148 yalikuwa ya ndani ya nchi na mashauri 31 yalikuwa ya nje ya nchi kati ya mashauri hayo yalijikita kwenye masuala ya mikataba ya ujenzi, uwekezaji na taratibu za manunuzi.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini aliwaagiza mawakili hao kwenda kuwa chachu katika kupunguza na kutatua migogoro ya uwekezaji katika sekta ya madini na rasilimali zote nchi.

Pia aliwataka kupunguza idadi ya mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na yanayoendelea kwa kuyamaliza kwa njia ya usuluhishi, ili kuimarisha juhudi za serikali katika kuwavutia wawekezaji na kutekeleza miradi mbalimbali nchi.

Pia, aliwaagiza kuishauri serikali na taasisi zake kikamilifu namna bora ya kumaliza migogoro na wananchi au wawekezaji bila kuathiri maslahi ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuwashauri waajiri kuhusiana na taratibu za uendeshaji wa mashauri pale wanapohitaji kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa umma.

Katika hatua nyingine aliwaasa mawakili hao kufuata kanuni za maadili ya utumishi wa umma kwa kuwa na tabia na mienendo inayozingatia utoaji wa huduma bora, utii kwa serikali, utoaji wa huduma bila upendeleo, kufanya kazi kwa uadilifu kuwajibika kwa umma na kuheshimu sheria za nchi.

# FAO, EU yafungua masoko kuwawezesha wakulima

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHIRIKA la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU), yameanzishwa mchakato wa kufungua masoko mapya manane ya kimataifa kwa ajili ya wakulima wadogo wa nanasi, pilipili manga, karafuu, kakao na vanila.

FAO na EU wanatekeleza mchakato huo kupitia Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea kwa Usalama wa Chakula Tanzania (STREPHIT).

Mradi huo hadi sasa umesaidia Tanzania kuongezeka kwa ufanisi katika shughuli za afya ya mimea na udhibiti wa viuatilifu, kuongezeka kwa uhakika wa chakula na malighafi ya viwanda, kupungua kwa uvamizi wa visumbufu vipya kutokana na kuimarika kwa uchunguzi wa visumbufu na kupungua kwa upotevu wa mazao kabla ya kuvunwa.

Jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, akifungua kikao kazi cha uandaaji wa nyaraka cha masoko mapya ya mazao hayo, alisema wadau mbalimbali, wakiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA), Wizara ya Viwanda na Biashara, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu Nchini (TOSC), Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) na FAO, wamekutana kwa siku tano katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, kutengeneza mambo mengine, urodha ya kitaifa ya visumbufu.

Katika kikao hicho, Mweli aliwakilishwa na Mratibu wa Taifa wa Miradi wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), Mdili Katemani.

"Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo FAO, tuweweka mikakati mbalimbali ya kupanua wigo wa masoko ya mazao kwenda nje ya nchi," alisema.

Sasa katika utaratibu wa viwango vya kimataifa ni kwamba ili uweze kufikia soko jipya lazima kwanza uandae kitu kinachoitwa 'Crop Pest Lists' yaani uwe na urodha ya kitaifa ya visumbufu vilivyoko nchini kwako, ambavyo vinaathiri zao hilo."

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, nyaraka hiyo inayoandaliwa itakuwa inaeleza kwa undani, jinsi uzalishaji wa zao husika unavyofanyika hapa nchini.

Mpango huo unalenga kulifikia soko lenye ukubwa wa Dola za Marekani bilioni 3.1 katika mazao hayo matano.

Ofisa Biashara wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Andrea Assenga, alisema kwa kuwa ni vigumu kutenganisha afya ya mimea na biashara ya kimataifa, Wizara hiyo itahakikisha inachangia kwa kiasi kikubwa kuboresha nyaraka inayoandaliwa, kwa kuzingatia mambo mbalimbali kama miongozo, ambayo imewekwa na Shirika la Biashara Duniani (WTO).



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), akiwaongoza viongozi wa Shirika la ECLAT Foundation na Upendo la Ujerumani, kukata utepe wa ujenzi wa kituo cha mafunzo, ujuzi na malezi kwa wasichana katika kijiji cha Emboreet, juzi. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala. **PICHA: GIFT THADEY**

## Wanafunzi wabuni mfumo kidijitali kuripoti ukatili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HOFU ya kukosekana usiri na usalama kwa waathirika wa unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika vyuo vya elimu ya juu na maeneo mengine nchini, imepata suluhisho baada ya wanafunzi wawili kubuni mfumo wa kielektroniki.

Mfumo huo pamoja na mambo mengine unazuia watu kusingizia watu wengine tuhuma za jinai.

Akizungumzia ubunifu huo wakati wa maonyesho ya ubunifu wa stadi za kazi kwa wanafunzi, yaliyohusisha wanafunzi zaidi ya 100, Neema Constantine ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa tatu anayesomea Shahada ya TEHAMA katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) alisema changamoto ya kuripoti matukio hayo kwa kutumia karatasi mtu anapokuwa polisi, inawafanya waathirika wengi kuficha taarifa au kughairi kutoa taarifa wakihofia usalama wao.

Kwa mujibu wa Neema, mfumo huo unamsaidia mwathirika mwenyewe kuripoti taarifa yake kwa haraka kwenda Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi bila kuhofia chochote, huku ukimhakikisha usiri na mtu haihitaji kuonekana au kwenda polisi.

"Sasa hivi watu wanaipitia changamoto hii kwa asilimia kubwa sana, kwa hiyo tulitamani kufanya hiki kwa sababu hapo nyuma njia ambazo zinatumika kuripoti hizi kesi, ni mifumo ya kiutamaduni; yaani mtu anaenda ofisini moja kwa moja, wakati mwingine kuna kuwa na mizunguko mingi mpaka kufikia kupata msaada," alisema.


Alisema watu wananyanyasika ila wanaogopa kutoa taarifa. Kwamba mfumo huu utamsaidia mtu kuripoti taarifa yake kwa haraka bila kuhofia chochote, inahakikisha kunakuwapo na usiri na mtu haihitaji kuonekana.

Mhadhiri MoCU, Dk. Cyril Komba, alisema baada ya serikali mwaka 2021 kuanzisha madawati ya kuripoti ukatili wa kijinsia kwenye vyuo vya elimu ya juu, wanafunzi hao walianza kazi ya kubuni mfumo utakaosaidia kupunguza matumizi ya karatasi.

Dk. Komba, alisema mfumo huo utasaidia kuondoa ukakasi au kumpa kazia mtu tuhuma.

Mkurugenzi wa Huduma za Wanafunzi wa MoCU, Dk. Elisifa Nnko, alisema maonyesho hayo ni ya 12 kufanyika chuoni hapo.

Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa MoCUSO, Yohana Kazimiri, aliishukuru menejimenti ya MoCU kwa kuruhusu wanafunzi wake kuonyesha vitu ambavyo wanavyo nje ya elimu ya darasani.





# Pambalu atangaza 'kumvaa' Wenje uchaguzi wa kanda

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

MWENYEKITI wa Baraza la Vijana Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA) Taifa, John Pambalu, ametangaza rasmi kutogombea nafasi hiyo.

Amesema malengo yake kwa sasa ni kuipata nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda ya Victoria.

Aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya nia yake ya kuongoza chama hicho ngazi ya Kanda ya Victoria baada ya kupita katika mchujo uliofanywa na Kamati Kuu ya chama hicho Taifa.

"Nimefanikiwa kuongoza katika nafasi mbalimbali kuanzia kata hadi taifa na sasa nataka kufanya makubwa zaidi nikiwa ngazi ya kanda kwa kwenda na vipaumbele sita nilivyoviweka katika neno la pamoja ambalo ni MUNOFU," alisema Pambalu.

Aidha, alisema neno hilo linasimamia maneno sita ambayo ni mafunzo kwa viongozi, uchaguzi mkuu na serikali za mitaa, nidhamu katika chama, operesheni za kisiasa husani vijijini, fursa kwa wote bila kujali hali za kielimu na ujenzi wa ofisi ya kanda.

"Kwa muda mrefu wanachama pamoja na viongozi wa kanda wamekosa fursa za mafunzo ili kuboresha utendaji kazi katika chama, hivyo kutokana na kuwa mimi ni mnufaika wa mafuzo lazima tuanze na kazi hiyo," alisema.

Aidha, alieleza kuwa kanda hiyo imekosa ofisi kwa muda mrefu, hivyo kupitia wanachama, wadau pamoja na wapenzi wa demokrasia watahakikisha wanajenga ofisi ya mfano kutokana na ukubwa wa kanda.

Kuhusu operesheni alisema atahakikisha anashiriki kikamilifu katika kuhamasisha mabadiliko katika kanda hiyo, ikiwa ni pamoja na kuanzisha operesheni za kisiasa hasa katika maeneo yaliyosahaulika.

Chadema kilianzisha mfumo wa uongozi kupitia kanda mwaka 2006 kwa kanda 10 ikiwa ni hatua kufuata utawala wa mfumo wa majimbo kama inavyotumika katika mataifa ya Kenya, Marekani, Ujerumani na Denmark, huku ukitajwa kuwa na mafanikio katika utawala.

Chama hicho tayari kimeruhusu mbio za kampeni katika uchaguzi huo kupitia mchujo uliofanywa na Kamati Kuu hivi karibu kwa kanda nne za kiutawala, huku Kanda ya Victoria John Pambalu akichuana na mtetezi wa nafasi hiyo, Ezekiel Wenje.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (kushoto), akimsikiliza Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Bia ya Serengeti, Neema Temba, alipomtembelea ofisini kwake, jijini Mwanza mwishoni mwa wiki. Kampuni hiyo, imekuwa ni mdau mkubwa wa maendeleo kwa kuchangia pato la mkoa huo na kusaidia miradi mbalimbali ya maji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANROADS yaendelea ukarabati miundombinu Tabora

**Na Benny Kingson,**
TABORA

WAKALA wa Barabara Nchini (TANROADS) mkoani Tabora, umesema unaendelea na ukarabati pamoja na maboresho ya miundombinu iliyoharibiwa na mvua.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Meneja wa TANROADS mkoani hapa, Raphael Mlimaji, wakati akiongea na Nipashe ofisini kwake kuhusu hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika kurejesha miundombinu hiyo.

Mlimaji alisema Mkoa wa Tabora haukuwa na athari kubwa za mvua bali ni baadhi ya maeneo ikiwa ni pamoja na Barabara ya Ipoe -Rungwa (km 9.2) na daraja linalounganisha barabara ambako ujenzi wake unaendelea.

Mlimaji alisema mkoa huo wenye mtandao wa barabara 37 na kati ya hizo 10 ni kuu na moja ya Ipole- Rungwa (km 172.42) ni ya changarawe, kwamba daraja lake ujenzi uliokuwa uishie Aprili mwaka huu na sasa utakamilika Juni, 2024.

Alitaja barabara nyingine zilizopata athari kuwa ni Ugala-Kaliua-Ulyankulu, Tabora-Kahama, Mwanange-Kaliua ambako tayari wamejaza mawe na vifusi ili ziendelee kutoa huduma.

Alisema Barabara ya Kalua-Lumbe (km 60) mkandarasi yupo kazini na Sh.bilioni 2.5 zimetolewa kutekeleza mradi huo pamoja na Barabara ya Bukumbi-Mudedo (km 24.39).

"Tumeomba Sh.milioni 16 kurekebisha maeneo korofi na pia taa 182 za barabarani zilizimika na zimeshushwa kutengenezwa na tayari tumewasiliana na TEMESA ili kuzifanyia matengenezo," alisema.

Vilevile alisema taa za kuongozea magari katika maeneo ya Mwafrika mjini nazo zilizimika na mkandarasi anaendelea kuzifanyia kazi.

## Waliopata ujauzito utotoni wapewa vyerehani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WASICHANA waliopata mimba za utotoni wakiwa shuleni katika Manispaa ya Shinyanga, wamepewa msaada wa vyerehani sambamba na mavunzo ya kuvitumia, lengo ni kuwawezesha kujitegemea na kujikwamua kiuchumi.

Akikabidhi msaada huo baada ya kuhitimu mafunzo yao katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), Meneja wa Shirika la Investing in Children and Society (ICS), Sabrina Majikata, alisema lengo la mradi huo ni kuimarisha uchumi na kuziishi ndoto zao.

"Tunao mabinti 75 kwa mkoa mzima ambao wapo kwenye vikundi, kikiwamo cha ufugaji, kilimo, pamoja na ushonaji ambao ni saba tumewapatia kila mmoja cherehani pamoja na vifaa vyote vya ushonaji ambazo zitawasaidia kutumia fani yao vizuri na kujikwamua kiuchumi," alisema Majikata.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, aliwasihi mabinti hao kufanya kazi kwa bidii pamoja na kuwa wabunifu ili wamudu soko kwenye ushindani.

Mmoja wa mabinti hao, Mary Willison ambaye alipata ujauzito akiwa kidato cha pili alisema mafunzo na msaada huo utamsaidia kujikwamua kiuchumi sambamba na kumtunza mtoto wake.

## Vijana milioni sita kufikiwa na elimu ya afya ya uzazi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIJANA zaidi ya milioni sita nchini wanatarajia kuelimishwa kuhusu afya ya uzazi na uchumi, lengo likiwa ni kuwaepusha na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na ngono zembe.

Hayo yalibainisha juzi na Meneja wa Kanda ya Magharibi wa Shirika la Girl Effect, Michael Luvanda, wakati wa uzinduzi wa jukwaa la 'Jibebe andaa kesho yako' uliofanyika katika viwanja vya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Alisema jukwaa hilo linalenga vijana wenye umri wa miaka 18 mpaka 29 pekee na watakuwa wakikutana kwa pamoja na kujadilii changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi katika jukwaa hilo.

Alisema watawafikia vijana milioni sita nchini na kati yao 300,000 wanatoka Wilaya ya Kahama na watawafikia kupitia mikusanyiko mbalimbali itakayokuwa inafanyika, mitandao ya kijamii pamoja na vyombo vya habari katika eneo husika.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, alisema kampeni hiyo imewafikishia elimu ya kujikinga na saratani ya mlango wa uzazi vijana 315, kati yao 35 wakipewa elimu ya uzazi wa mpango na 30 wakipewa chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo.

Ofisa Tarafa wa Isagehe, Vicent Ndesekio alisema, utoaji wa elimu ya kijikwamua kiuchumi uendane na njia ya upatikanaji wa mikopo isiyokuwa na riba, ili vijana hao wasiingie katika mikopo umiza.



Ukurasa 12

**Nchimbi alivyomaliza kigugumizi cha mahindi, mikopo ya kahawa**



Ukurasa 13

Rais Mwinyi na Zanzibar mpya inayong'ara kiuchumi, kisiasa





Ukurasa 14

**KIFO CHA RAISI**

**Kilio wanaharakati Mashariki ya Kati**


# siasa

JUMATANO MEI 22, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


KIONAMBALI CCM KINANA:

# Wasichukulie poa uchaguzi unaokuja hautakuwa 'kitonga'

• Aonya wasiparamiwe kwenye mikutano

**Na Maulid Mmbaga**

WAKATI ikiwa imebakia miezi kadhaa kufanyika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofuatiwa na Uchaguzi Mkuu wa 2025 wana CCM wamepewa tahadhari.

Ujumbe ulioko ni kwamba wasiichukulie michakato hiyo kwa wepesi, kwa kuwa haitakuwa rahisi au mteremko.

Angalizo lake Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, akiwaasa wanachama wake kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu utakuwa na ushindani hivyo wasibwete, badala yake wawe na umoja na mshikamano kufikia ushindi.

Yanajiri akiwa mkoani Mara katika ziara ya kukagua maendeleo ya chama hicho na kusisitiza umuhimu wa uadilifu kwa chama na kuachana na kukipigania ili kupata ushindi na kuachana na undumila kuwili.

Aidha, anasisitiza viongozi kufuata maadili ya uchaguzi pamoja na kufanya kila linalowezekana ili waibuke na ushindi licha ya uchaguzi huo kuonekana kuwa na ushindani zaidi.

"Zile sheria za uchaguzi zilizotungwa bungeni zinatoa nafasi ya ushindani, kwa hiyo msibweteke, badala yake tujipange kikamilifu ili tupate ushindi wa kishindo mwaka huu pamoja na uchaguzi mkuu wa mwaka ujao," asesema Kinana.

Anawaambia "Kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa ni vyema wana CCM tukashikamana na kama kuna mtu mchana yuko upande wa CCM na usiku upinzani anapaswa kuwekwa kando haraka."

"Hatuwezi kukubali watu wavae sare za kijani mchana halafu baadaye wanabadilika, kama kuna changamoto yoyote mnapaswa kuzizungumza kama chama ili kupata ufumbuzi. Tunatakiwa tushikamane na tuzingatie kanuni na katiba yetu ya chama," anaongeza.

Kuhusu viongozi ambao wamechaguliwa na sasa wako madarakani wakiwamo madiwani na wabunge, Kinana anasema waachwe wafanye kazi akieleza kuwa hakuna sababu ya kuwavuruga, kwa kuwa kipindi cha uchaguzi bado hakijafika akikumbusha kuheshimiwa kwa kanuni za chama hicho.

"Kuna watu wanaitwa madalali wa vyeo, kazi yao ni kuuza vyeo anakuja kwako anakwambia mwaka ujao unatakiwa tukuchague wewe, ukisikia hivyo ujue anatafuta riziki na akimaliza kuzungumza anaomba nauli, ujue huyo ni dalali.

"Wakati mwingine anakupigia simu anakwambia hebu nirushie bando kuna habari nataka nikupe, hao ni madalali, ukija kuanguka anasema mimi nilikusaidia ila wajumbe wamekuangusha," anakumbusha Kinana.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, akizungumza na wana CCM wa Mkoa wa Mara. **PICHA: MAULID MMBAGA**

### UKABILA ACHENI

Makamu Mwenyekiti Bara, anawasisitiza wanachama Watanzania kuachana na ukabila akieleza kuwa ni mambo ya kizamani na yanawagawa watu, jamii pamoja na taifa.

Kinana anasisitiza hayo baada ya baadhi ya wanachama wa chama hicho wilayani Rorya, mkoani Mara kuibua hoja kwamba kuna mambo yanafanyika wilayani hapo ambayo yanaashiria kuwepo kwa changamoto ya ukabila miongoni mwao.

Anawaambia Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere anatoka Mkoa wa Mara, na ni kabila dogo lakini ameongoza nchi kwa miaka 24, na kwamba alipendwa, aliheshimiwa, alithaminiwa na alitukuzwa sio kwa sababu ya ukabila bali ni kazi aliyokuwa anafanya, utendaji na uadilifu wake uliomfanya aheshimike Tanzania, Afrika na duniani.

"Sasa usimpe mtu nafasi ya uongozi sababu ya kabila lake, dini au umbile usimhukumu, hayo ni mambo ya kizamani sana, tuangalie mtu ana uwezo atafanya kazi, atajituma na kujitolea? Mnampima kwa vigezo sio kwamba huyu ni ndugu yangu.

"Mtu mmoja kwenye kabila lako akipata cheo anakusaidia nini? Uko kijijini kule mngekuwa mnagawana mshahara sawa, kila mmoja anakuletea 300,000 kutoka kwenye mshahara wake kwasababu ni kabila lako sawa. Wekeni watu wenye uwezo kuwa viongozi," anasisitiza Kinana.

Aidha, anaeleza kuwa jambo ambalo Baba wa Taifa aliwaachia ni umoja wa kitaifa, akitolea mfano kwamba kuna nchi bila kuzibainisha kwa majina, mtu hawezi kuwa gavana wa jimbo kama anatoka sehemu nyingine, lakini Tanzania wanafanya kazi nchi nzima.

Anaendelea kusisitiza wana CCM kuwa na umoja katika utendaji akihadharisha kwamba wasiposhikamana kutakuwa na tatizo, na kwamba miundo na mifumo ikifanya kazi kikamilifu chama kitaendelea kuwa na nguvu, kitaaminika na kukubalika.

Anasema chama hicho kinaendeshwa kwa utaratibu, kwa kufuata katiba, na pia kina kanuni kwa kila jambo ikiwamo uchaguzi, maadili na kanuni za utumishi, akisisitiza kuwa ndani ya CCM kila kitu kinaangaliwa na kinaandikwa.

"Ukiona mtu anafanya vitu visivyokuwa sawa hayo ni yake, pia tunaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, ili tushinde vizuri viongozi lazima mtende haki, msipandikize watu na msipokee rushwa kwani ni adui wa maendeleo," amesema Kinana.

### ASIPENDELEWE MTU

Kinana anawageukia viongozi, akiwaambia wasiwapendelee wagombea, wala kupandikiza watu na kuacha kununuliwa kwa kupokea rushwa, badala yake watende haki kwa kuwa kila mmoja anahaki sawa kwenye uchaguzi.


**INAENDELEA UK. 14**

# Nchimbi alivyomaliza kigugumizi cha mahindi, mikopo ya kahawa



Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Emmanuel Nchimbi akiweka shada la maua katika kaburi la mwasisi na mpigania uhuru Constantine Millinga. **PICHA: HALFANI CHUSI**

**Na Halfani Chusi**

ZIARA ya Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, mkoani Ruvuma, wakati wakulima wakikabiliwa na ukosefu wa masoko ya mahindi na mikopo, imegeuka tiba baada ya kiongozi huyo kuleta ufumbuzi na tumaini jipya.

Ni ziara iliyokuwa na dhima ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi na ikiwaacha wakulima na tabasamu, hasa Mbinga.

Akiongozana na Katibu wa NEC -Oganaizesheni Issa Haji Gavu na Katibu wa NEC- Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa Amos Makalla, Balozi Nchimbi, anatembelea mikoa sita, akihitimisha safari mkoani Ruvuma.

Malalamiko ya wananchi ya kukosa soko la mahindi, anakutana nayo mjini Mbinga, wakieleza kuwa hawakupata pakuuzia mahindi tangu mwaka jana na pia wakazungumzia ukosefu wa mikopo kwa wakulima wa kahawa.

Akijibu kilio chao, Dk. Nchimbi, anawasiliana na Waziri wa Kilimo Hussein Bashe,ambaye anawahakikishia wakulima hao kuwa serikali itafungua maghala mengine na kununua mahindi yote kwa bei nzuri na kuwataka wasiwe na hofu.

"Mahindi yaliyobaki mwaka jana tutayanunua na ya msimu huu mpya pia tena kwa bei nzuri.

> "Urithi pekee ambao baba alituachia alituambia isitokee hata mtoto mmoja akahama CCM, alikuwa mzalendo, mpambanaji na mwenye ushawishi mkubwa.

Ruzuku ya mbolea itaendelea kutolewa kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan, ameelekeza, kwahiyo baada ya malipo hayo Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA), utafungua maghala kuchukua mahindi yote." Anaahidi Bashe.

Anavikataza vyama vya ushirika kukopa fedha kisha jukumu la kulipa deni linabaki kwa wakulima akionya kuwa si haki.

"Tunakwenda kupitia mfumo na tunapiga marufuku vyama vya ushirika kukopa fedha halafu mwisho mkulima anapeleka kahawa hapokei fedha kumbe chama chake kilichukua fedha bila kumhusisha" anaonya Bashe.

Anatolea ufafanuzi wa gharama za magunia akisema mpango walionao baada ya Bunge la Bajeti watatangaza mfumo mpya wa kugharamia na kuuza kahawa ambao utafanya iuzwe kwenye vyama vya msingi badala ya chama kikuu kujikusanyia na kufanya uamuzi.

Baada ya maelezo ya Bashe Nchimbi anawataka wananchi kuwa na imani na CCM akiahidi kuendelea kuisimamia serikali kuhakikisha kero za Watanzania zinatatuliwa kwa wakati.

Anawataka wana chama kuchagua wagombea waadilifu wanaoheshimu watu na walio tayari kutumikia ili kujenga taifa kwa weledi.

"Kila taasisi inafanya kazi vizuri, fundi cherehani aliyefanya kazi kwa miaka 10 lazima atakuwa mahiri hawezi kulinganishwa na mtu asiye na uzoefu. Kila inapotokea nafasi ya uchaguzi kumbukeni wapinzani ni wazuri kuendelea kuwa wapinzani na CCM ni bora kuendelea kuongoza nchi kila mmoja mpe nafasi kwa uzoefu wake."

Katibu wa Oganaizesheni Taifa, Issa Gavu katika mkutano huo, anawataka wananchi kujitokeza kuwachagua viongozi wa chama hicho mwaka huu na mwakani.

Hakuna viongozi wanaoweza kuliletea taifa mafanikio nje na viongozi walioko ndani ya CCM, hivyo wananchi wafanye uamuzi sahihi kipindi cha uchaguzi kitakapofika, anasema.

"Ninaomba muda ukifika jiandikisheni kwenye daftari la wapiga kura, ili tushinde katika uchaguzi ulio mbele yetu, jitokezeni na kupiga kura kuendeleza umoja na mshikamano ndani ya chama chetu."

Katibu wa Itikadi Uenezi na Mafunzo Taifa, Amosi Makalla, anasema lengo la ziara yao ni kuangalia uhai wa chama, utekelezaji wa ilani, maandalizi ya uchaguzi na utatuzi wa kero za wananchi.

"Mpaka kufikia leo tunahitimisha ziara yetu tuliyoifanya katika mikoa sita tumesikiliza na kutatua kero zaidi ya 100 kwa njia ya kisayansi (kimyakimya) lakini tumeridhishwa na namna mabalozi wa chama chetu wanavyofanya kazi ya kuimarisha CCM niwaombe tuendelee." Anasema.

Mbali na kusikiliza na kutatua kero za wananchi pia, Balozi Nchimbi na viongozi wenzake walilizuru kaburi la marehemu John Komba aliyewahi kuwa mbunge wa Mbinga na mhamasishaji wa nyimbo wa bendi ya TOT ya CCM.

Dk.Nchimbi anaeleza kuwa chama kitaendelea kuenzi na kukumbuka mchango wa Komba akikimbusha kuwa alishiriki kuandaa taifa, vita ya Uganda, kutunga nyimbo ambazo zimechangia vijana wengi kujiunga na CCM.

Akiwashukuru viongozi wa CCM , kwa faraja, familia ya Komba, ikiongozwa na mtoto wake George Komba, anakishukuru chama hicho kwa kukumbuka mchango wa baba yao, akieleza kuwa wamefarijika sana.

Anakumbushia kuwa baba yake alikuwa mwanajeshi na jasiri aliyepambana kukiongoza chama hicho kupata ushindi. Anaahidi kwamba familia hiyo itaendelea kushiriki katika uchaguzi wa mwaka huu na mwakani.

"Urithi pekee ambao baba alituachia alituambia isitokee hata mtoto mmoja akahama CCM, alikuwa mzalendo, mpambanaji na mwenye ushawishi mkubwa."

Aidha, viongozi hao walizuru kaburi la hayati Mzee Constantine Millinga, aliyekuwa mmoja wa waasisi na wapigania uhuru kuanzia wakati wa Tanganyika African Association (TAA),TANU, hadi CCM katika makaburi ya familia yaliyopo, mtaa wa Mhekela, Mbinga Mjini.

Mbali ya kuweka shada ya maua, wanakutana na mjane wa Millinga, Maria Mapunda (88), na kushiriki ibada ya kumuombea iliyoongozwa na Padri Andrea Silimbo.

Mzee Millinga alikuwa mmoja wa viongozi waandamizi wa TAA, TANU hadi CCM, alishirikiana na wenzake, wakiwemo viongozi wakuu na wanachama, wakiongozwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, akiwa sehemu ya waasisi wa vyama hivyo vya ukombozi vilivyobeba chimbuko na kuweka misingi ya uhuru na maendeleo ya Tanganyika, baadaye kuipata Tanzania, na kuzaliwa kwa CCM, alifariki dunia Machi 5, 2018.

Akizungumza wakati wa kutoa salaam za pole kwa wanafamilia na wananchi wengine, Dk Nchimbi anaahidi kama ilivyokuwa kwa Komba kuwa CCM itaendelea kuenzi na kujifunza kupitia mema yaliyofanywa na waasisi wake.

Ziara hiyo iliwafikisha viongozi hao mikoa ya Katavi,Rukwa,Songwe, Mbeya, Njombe na kuhitimishiwa Ruvuma.

# Rais Mwinyi na Zanzibar mpya inayong'ara kiuchumi, kisiasa

**Na Deogratias Mutungi**

GEORGE Washington Rais wa zamani wa Marekani pamoja na Kwame Nkrumah, wa Ghana kwa nyakati tofauti walikuwa wanaongea jambo moja, ni kutoa kauli zinazolandana kuhusu kuwapa sifa viongozi wanaostahili haki hiyo.

Wanataka kuwatetea na kuwalinda kihoja na kumtia moyo kiongozi wa nchi anayejitoa kizalendo kuwatumikia raia wake.

Washington na Nkrumah wanasema isitokee mtu akaogopa kusema ukweli na kuwatetea viongozi wenye nia njema na raia wao.

Kwa mstakabali huo, Rais Hussein Mwinyi, anastahili kulindwa kwa hoja kuhusu ubora na ufanisi katika utumishi kwa Wazanzibari.

Ukirejea hotuba ya Rais Mwinyi, aliyoitoa Januari 24, kwenye maandalizi ya sherehe za Muungano mwaka huu, akiwa Zanzibar, mafanikio ya awamu yake yanabainishwa.

Ufanisi wa kiutendaji wa rais huyo wa awamu ya nane katika kuwatumikia Wazanzibari, unaanza kuonekana kwenye kuongeza pato halisi la taifa kwa mwaka ikiwa mwaka 2020 lilikuwa Shilingi trilioni 3.166, lakini mwaka 2022 liliongezeka na kufikia Shilingi trilioni 3.5.

Inawezekana mwananchi wa kawaida akajiuliza ni zipi faida za pato la taifa na zina umuhimu gani kwake?

Kwanza pato la taifa hutoa picha ya ukuaji wa uchumi wa nchi, pia takwimu za mapato ya taifa hufanikisha kutunga sera za kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya sekta zote.

Ni wazi kuwa maendeleo hayo yatamgusa mwananchi wa kawaida katika kupata huduma muhimu za kiafya, kielimu na miundombinu, hivyo kuwa ndani ya mafanikio.

Aidha, hotuba yake inachambua jinsi Rais Mwinyi alivyofanikiwa kuimarisha njia za ukusanyaji wa mapato kutoka bilioni 790.48 mwaka 2020-2021 hadi kufikia trilioni 1.4 kwa mwaka 2022-2023.

Hiyo ni hatua kubwa sana katika maendeleo ya Wazanzibari kiuchumi na fursa mbadala ya kupanua wigo wa wananchi kuhudumiwa kimaendeleo kwa wepesi zaidi.

Udhaifu wa serikali yoyote huwa katika kuhimili ukusanyaji kodi wakati serikali madhubuti na imara hujitambulisha katika kukusanya kodi kwa misingi ya maendeleo ya nchi na watu wake.

Uimara, ubora na uwajibikaji wa Rais Mwinyi ni pamoja na eneo hili la kukusanya mapato ya taifa kikamilifu na kwa ufanisi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, **PICHA: MAKTABA**

Rais Mwinyi ameing'arisha Zanzibar kiuchumi, kwenye ongezeko la ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.8 kwa mwaka 2022-2023 ikilinganishwa na asilimia 1.3 ya mwaka 2020.

Katika hotuba yake anaeleza kuwa uchumi wa Zanzibar unakuwa kutokana na uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kipaumbele, ikiwa ni pamoja na miundo mbinu ya barabara, bandari, viwanja vya ndege na huduma za maji safi na salama.

Sambamba na hilo, pato la mtu binafsi limeongezeka kutoka Shilingi milioni 2.5 kwa mwaka 2020 na kufikia Shilingi milioni 2.8 mwaka 2022.

Hotuba ya Mwinyi, inabainisha kuwa serikali ya awamu ya nane imefanikiwa kudhibiti mfumuko wa bei na kuendelea kuwa katika tarakimu moja, ambapo kwa mwaka 2023, ulikuwa ni wa wastani wa asilimia 6.8.

Ni faida kiuchumi kama mfumuko wa bei ni mdogo, usioyumba na unaobashirika.Zipo faida za mfumuko wa bei ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wanunuzi na wazalishaji kuweka mipango na mikakati ya muda mrefu bila kuhofia mabadiliko ya bei.

Aidha, wachumi wanasema kuwa mnunuzi anakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa kwa bei iliyopo.

Pia mfumuko wa bei ambao ni imara na unaotabirika husaidia kukua uchumi kwa kuongeza kasi ya uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali.

Kwenye eneo la uwekezaji, miradi 296 yenye thamani ya Dola bilioni 4.5 (sawa na Shilingi trilioni 11.6) imeidhinishwa, miradi hiyo inakadiriwa kutoa ajira 17,479 ikihusisha uwekezaji katika visiwa vidogo 16 wenye thamani ya Dola milioni 377.5 zaidi ya Shilingi bilioni 971.

Kwa upadne wa visiwa vidogo vipo 52 na kwa miaka 60 ya Mapinduzi vilikuwa havijatumika kwa maendeleo wala kuleta tija kwa taifa licha ya kutumiwa na wavuvi wanaoishi kwenye makambi kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Baada ya uongozi wa serikali ya awamu ya nane kuingia madaraka ikihamasisha sera ya uchumi wa bluu imevikodisha visiwa 16 ili kukuza uwekezaji na kupata mapato vikiendeelezwa kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Visiwa hivyo vilivyoko Unguja na Pemba , vinapotumika kuleta maendeleo ni mafanikio makubwa katika kukuza uchumi wa nchi kuanzia uwekezaji wa hoteli za kitalii na miradi mingine na kwamba jumla ya miradi yote iliyoekezwa katika sekta hiyo ya utalii ni 112 serikali ikitegemea kuvuna Dola 300,000,000 zaidi ya Shilingi bilioni 773.

> Rais Mwinyi ameing'arisha Zanzibar kiuchumi, kwenye ongezeko la ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.8 kwa mwaka 2022-2023 ikilinganishwa na asilimia 1.3 ya mwaka 2020.

Kadhalika upo ujenzi wa viwanda 36, mambo yanayoonyesha kuwa Zanzibar chini ya Rais Mwinyi inanoga na kufana katika kuimarisha mazingira ya kufanya biashara, ambapo kwa mwaka 2022 Zanzibar imefanya biashara yenye thamani ya shilingi trilioni 1.4 ukilinganisha na bilioni 913.1 za mwaka 2020, hili ni sawa na ongezeko la asilimia 57.6

Kwa muhtasari hotuba inatoa takwimu zinazoonyesha namna serikali ya awamu ya nane ilivyojipanga kufanya mabadiliko na kuleta njia na dira ya kiuchumi.

Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kiongozi shupavu ni yule anayeonyesha njia ya mafanikio, jambo ambalo Rais Mwinyi amelifanya na anastahili kupewa sifa zake.

Hayo ni mafanikio makubwa kwa kiongozi mwenye dhamana kama rais wa nchi akianza kuonyesha utumishi uliotukuka kwa watu wa Zanzibar na Tanzania pia.

Wazanzibari, ni vyema kuwapa mrejesho wa mafanikio na changamoto katika utumishi wa umma.

KIFO CHA RAISI

# Kilio wanaharakati Mashariki ya Kati

## •Urusi, Pakistan wamlilia, Magharibi wakaa kimya

**Na Mwandishi Wetu**

KIFO cha Rais wa Iran, Ebrahim Raisolsadati maarufu, Ebrahim Raisi (63), kinatajwa kuwa pigo si kwa Wairan pekee bali makundi mbalimbali ya Kiislamu Mashariki ya Kati.

Pigo hilo linatokana na ukweli kuwa Raisi alikuwa na msimamo mkali wa kuyaunga mkono, lakini alikuwa mshirika wa Urusi, Syria kadhalika aliyabeba makundi ya wapiganaji ya Lebanon, Yemen na Palestina.

Rais wa Iran alipoteza maisha pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje, Amir Abdollahian baada ya helikopta waliyopanda kuanguka juzi ikidaiwa chanzo ni hali mbaya ya hewa, ikiwa katika anga la Azerbaijan, wakati wakirejea Teheran baada ya mkutano na mwenzake Ilham Aliyev wa Azerbaijan.

Baadhi ya mataifa ya Kiislamu wameita kifo hicho kama 'hasara kubwa' huku yakitangaza siku za maombolezo ya kitaifa.

Waziri Mkuu wa Pakistan, Shehbaz Sharif, amesema kifo cha Raisi ni 'hasara kubwa'.

Pakistani imetangaza siku moja ya maombolezo na Lebanon ikitangaza siku tatu.

Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu, Mohammed bin Zayed Al Nahyan, anasema nchi yake inasimama na Iran wakati huu wa majonzi, wakati Rais Nicolás Maduro wa Venezuela, akimtaja Raisi kama kiongozi wa kipekee.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi, Sergei Lavrov, anasema Raisi alikuwa rafiki wa kweli na wa kutegemewa wa Urusi.

Rais wa Syria, Bashar al-Assad ameeleza kuumizwa na kifo hicho. Iran imekuwa ikiunga mkono utawala wa Assad ambao umekumbwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa muda mrefu sasa.

Rais wa Urusi, Vladimir Putin, wa China, Xi Jinping, wa Misri, Abdel Fattah El-Sisi na wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, wametuma salamu za rambirambi, wakati mataifa ya Magharibi yanayoiunga mkono Israel yakiwa kimya.

Rais alianza kuongoza Iran 2021, baada ya kushinda uchaguzi, akiingia madarakani kutoka mhimili wa mahakama. Ni mzaliwa wa mji wa Mashhad na alisifika kuwa kiongozi mwenye ushawishi mkubwa Iran na ndani ya mataifa ya Kiislamu. Kadhalika



Rais wa Iran Ebrahim Raisi (kulia) na Waziri wa Mambo ya Nje Hossein Amir-Abdollahian, enzi za uhai wao. **PICHA: BBC**

**MAKUNDI YAMLILIA**

Iran ni mshirika wa makundi ya kiharakati Mashariki ya Kati likiwamo la wanamgambo la Hezbollah nchini Lebanon, inatajwa kulipatia kundi hilo msaada wa kifedha na kijeshi wakati wa utawala wa Israel wa Lebanon katika miaka ya mwanzoni mwa 1980 na kama kikosi cha kuwatetea Washia wa Lebanon.

Wahouthi, wanaharakati walioko Yemen waliofadhiliwa pia na Iran ni miongoni mwa wale wanaotetea Palestina na kuipinga Israel.

Aidha, kundi la Hamas la Palestina linalopambana katika ukanda wa Gaza kuidhibiti Israel, liliungwa mkono na Iran na katika siku za hivi karibuni, Raisi alituma makombora Israel kama ishara ya kuipinga kuwaua Wapalestina na kuonyesha kuunga mkono Hamas.

Hezbollah, Houthi na Hamas, yanatajwa kuwa na nguvu za kijeshi na kisiasa kwa madai ya kuungwa mkono na Iran.

Raisi alikuwa kiongozi namba mbili kwa vile katiba inaelekeza kuwa Mkuu wa Nchi ni Seyyed Ali Hosseini Khamenei (85), na pia ndiye mwenye uamuzi wa mwisho katika masuala yote ya kimkakati.

Wachambuzi wa masuala ya siasa za Mashariki ya Kati, wameviambia vyombo vya habari vya kimataifa kuwa Raisi, aliyekuwa na msimamo mkali, alikuwa akiandaliwa kuwa Kiongozi Mkuu wa Iran baada ya Khamenei.

Wanaeleza kuwa kifo chake ni pigo la kuanza maandalizi mapya ya mrithi wa madaraka hayo ya juu ya nchi na pia rais wa nchi kwenye uchaguzi ujao.

Shirika la Habari la Reuters, linalochambua uongozi wa Iran, linasema Raisi alikuwa chaguo wa kwanza la Wairan na Khamenei kuwa mkuu wa nchi.

"Kufariki ghafla kwa Raisi kumezua gumzo la nani hatimaye atachukua nafasi ya kiongozi mkuu Khamenei ambaye afya yake imekuwa gumzo kwa muda mrefu," linaongeza.

Kuondoka kwa Raisi hakutarajiwi kuvuruga mwelekeo wa sera ya Iran au kuitikisa nchi hiyo kwa njia yoyote, inaongeza Reuters.

"Lakini itakuwa majaribu kwa mfumo ambao watu wenye msimamo mkali wa kihafidhina sasa wanatawala maeneo yote ya mamlaka, waliochaguliwa na ambao hawajachaguliwa. Wapinzani wake watafurahishwa na kuondoka kwake hasa kwa kuwa anatuhumiwa kuhusika na mauaji ya wafungwa wa kisiasa miaka ya 1980 alipokuwa mwendesha mashtaka," linafafanua.

Mazishi yake ya kiserikali yaliyofanyika jana mjini Tabriz yalijaa hisia na kutoa fursa kwa wahafidhina kueleza watakavyoendelea kusimamia nchi hiyo inachokiamini.

Baada ya kuthibitika kwa kifo hicho, Khamenei alitangaza siku tano za maombolezo ya kitaifa huku nchi jirani zikitangaza pia maombolezo.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Ali Bagheri Kani, ndiye anayeiongoza wizara hiyo kufuatia kifo cha Hossein Amir-Abdollahian wakati Makamu wa Kwanza wa Rais, Mohammad Mokhber, amechukua nafasi ya Raisi ambayo ataitumikia kwa siku 50 kabla ya uchaguzi.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi, Sergei Lavrov, anasema Raisi alikuwa rafiki wa kweli na wa kutegemewa wa Urusi.

Nchi za Magharibi zinaishutumu Iran kwa kutuma mara kwa mara ndege zisizo na rubani kwa Urusi ili kuzitumia katika vita vyake dhidi ya Ukraine, shutuma ambazo Iran imesema ilitoa 'idadi ndogo' ya ndege zisizo na rubani kwa Urusi kabla ya vita kuanza Februari 2022.

**MOHAMMAD MOKHEBER**

Huyu ndiye aliyekuwa makamu wa kwanza wa rais ambaye sasa amekaimu kiti cha urais, akiwa na miaka 68, alichaguliwa kuwa makamu wa kwanza wa rais kwenye uchaguzi wa 2021 ambao marehemu Raisi aliingia madarakani.

Ni mwanadiplomasia ambaye yuko karibu na Kiongozi Mkuu wa Iran, Ali Khamenei na sasa anakuwa sehemu ya baraza la watu watatu litakaloandaa uchaguzi mpya wa rais katika muda wa siku 50 zijazo.

*VOA, REUTERS, BBC*

# Wasichukulie poa uchaguzi unaokuja hautakuwa 'kitonga'

**INATOKA UK. 11**

"Mtu anakwenda mahali anawatafuta watu anawakusanya, anamtafuta mwenyekiti wa mtaa au kijiji wanakaa kikao kikimalizika wajumbe wanauliza sasa unatuachaje? Rushwa ni adui wa haki, inaathiri maendeleo ya taifa letu, anaopokea na anaetoa rushwa anafanya kosa kubwa. Mbaya zaidi ni yule anayedai anasema usiponipa tutakutana kwenye chaguzi sio sawa jamani.

"Mtu anakupa fedha halafu anafanya uongozi wa miaka mitano anakusaidia nini? Kwa hiyo angalia kiongozi kazi anayoifanyia jamii siyo atakusaidia nini wewe binafsi, kiongozi anayepita kwa rushwa akishapata nafasi hatakujali, kwasababu nafasi ile kainunua, hiyo ndio siri, tendeni haki zingatieni katiba na kanuni ili tupate viongozi wazuri," anasisitiza Kinana.

Vile vile, anaeleza kuwa kiongozi bora ni yule anayepatikana kwa uadilifu, akieleza kuwa wanawategemea wazee kutoa maoni, kuwaongoza, kuwapatanisha pale ambapo wameharibikiwa.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mara, Agnes Marwa, anasema viongozi katika mkoa huo wanafanya kazi na wanatekeleza ilani ya chama, licha ya kwamba tofauti ndogo ndogo haziwezi kukosekana.

Anawasisitiza wanachama kuacha kufanya kazi na watu wa nje badala yake waungane na viongozi walioko madarakani, wakisubiri muda wa uchaguzi ufike ili wachuje wenyewe ni nani wanayetaka kubaki naye.

YOTE YANA MWISHO

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) Mkoa wa Simiyu, Emmanuel Silanga, anawakumbusha viongozi kuwa kila kiongozi katika nafasi yake, ubunge na udiwani itafika muda utaisha na itatangazwa, wanachama wataomba na mwenye sifa atachaguliwa.

Anasisitiza kwamba kwa wale watakaopewa nafasi wafanye kazi ya chama na wasianze kusumbuana na watu wengine. Akibainisha kuwa kuna baadhi ya watu ni wabishi, hawawezi kukubali kwamba wameshindwa na kusistiza kukubali kuwa kila jambo linamwisho.



## TRA yajivunia makusanyo kupaa miaka 3 ya Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Dodoma imeongeza wastani wa ukusanyaji kodi kutoka Sh.bilioni 15.19 hadi Sh.bilioni 18. 71 katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu mafanikio ya mamlaka hiyo jijini hapa, Meneja wa TRA, Mwita Ayubu, alisema mafanikio hayo ya makusanyo yametokana na uboreshaji wa uhusiano kati yao na walipakodi.

Alisema kuwa mwaka 2021 Mkoa wa Dodoma ulikuwa na wafanyabiashara 3,812 wanaotumia mashine ya EFD, hivi sasa wameongezeka na kufikia 9,367 ikiwa ni ongezeko la wafanyabiashara 5,555.

"Mengine yaliyowezesha kupanda kwa kiasi hicho cha fedha cha ukusanyaji ni ongezeko la uwekezaji na ukuaji wa shughuli za kiuchumi ikiwamo uzalishaji viwanda na sekta za ujenzi na usafirishaji na uhamasishaji kwa kupitia elimu kwa mlipakodi," alisema.

Alibainisha kuwa pia ongezeko la matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usimamizi wa kodi kutoka kwa wananchi kwa kulipa kodi kwa hiari, kuongezeka kwa hamasa ya ulipaji kodi kutoka kwa wananchi kwa kuona matumizi sahihi ya kodi wanazolipa.

Hivyo, aliwasisitiza wafanyabiashara kutumia mashine za EFD kutokana na kuwapo kwa faida kama vile uboreshaji wa kumbukumbu za biashara kwa njia za elektroniki ambayo ni salama na ya kuaminika.

Hata hivyo, alisema mamlaka hiyo inakabiliana na tatizo la kuongezeka kwa wimbi la matumizi ya stempu za kielektroniki za kughushi kwa walipakodi, hali inayosababisha upotevu mkubwa wa mapato.

# Dk. Mpango atoa maagizo 10 uimarishaji asali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa maagizo 10 yatakayowezesha uimarishaji wa asali nchini, mojawapo ni balozi zote kujizatiti kutafuta masoko ya bidhaa zitokanazo na nyuki ili kusaidia taifa kupata fedha za kigeni na kujiimarisha kiuchumi.

Alitoa maagizo hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akifunga maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani iliyofanyika kitaifa mkoani Dodoma.

Alisema balozi zote zinapaswa kutafuta masoko ya bidhaa zitokanazo na nyuki ili kusaidia kupatikana kwa soko la uhakika kwa wafugaji nyuki nchini.

"Lakini pia naagiza Wizara ya Fedha kupunguza kodi kwenye bidhaa zinazotumika kwenye uchakataji wa asali pamoja na vifungashio ili kutoa ahuweni kwa wazalishaji wa bidhaa zitokanazo na mazao ya nyuki nchini," alisema Dk. Mpango.

Kadhalika, alisema pamoja na uwepo wa maeneo makubwa ya misitu na uoto wa asili nchini bado uzalishaji wa asali upo chini, hivyo aliiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI) kufanya tathmini ya uwezo wa uzalishaji wa asali ulipo kwa sasa nchini.

Pia katika maelekezo yake aliitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI kuyatambua maeneo maalum yenye fursa za kipekee katika eneo la Mkoa wa Dodoma na Singida ili kuyahifadhi kisheria.

Aidha, aliitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kushirikiana na wadau wa sekta hiyo kuja na mpango maalum wa ufugaji wa nyuki, ikiwamo kuendeleza programu ya upandaji miti.

Agizo lingine ni TAMISEMI kupitia halmashauri zake zenye fursa ya ufugaji nyuki kote nchini kuajiri wataalamu watakaotoa huduma ya ugani kwa wananchi na wizara inayohusika na kilimo kuandaa mkakati wa uchavushaji katika mazao ili kuongeza uzalishaji. Vile vile, alivitaka vyuo vya mafunzo ya nyuki nchini kikiwamo Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kuwatumia wajasiriamali wanaofanya vizuri katika sekta hiyo, ili kuwafundisha wadau wengi zaidi.

Awali, Waziri wa Maliasili na Utalii, Angelah Kairuki, alisema sekta hiyo kupitia nyuki imekuwa na mchango mkubwa katika eneo la uzalishaji wa mazao ya chakula.

Alisema matokeo ya utafiti zilizofanyika nchini zinaonesha kuwa zaidi asilimia 80 ya mimea ya chakula inayolimwa hapa nchini huchavushwa na nyuki.

Mkurugenzi wa Kijiji cha Nyuki, Phillemon Kihemi, alisema moja kati kero zinazowakabili wafugaji nyuki nchini ni uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za kibinadamu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (wa tatu kushoto), kuhusu huduma za teknolojia na mawasiliano zinazotolewa na Vodacom Tanzania, alipotembelea banda la kampuni hiyo, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Uhusiano wa kampuni hiyo, Zuweina Farah. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tume yataja sababu kuletwa roboti Eunice

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SIKU chache baada ya roboti Eunice kuwa gumzo katika mitandao ya kijamii, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA nchini, Dk. Nkundwe Mwasaga, amesema lengo la kuleta roboti hiyo ni kuimarisha ubunifu wa kidigitali katika kukuza uchumi wa taifa.

Akizungumza na Nipashe, Dk.Mwasaga alisema teknolojia ya roboti inaweza kusaidia katika majukumu mbalimbali ikiwamo ajali inapotokea.

"Huu ni ubunifu ambao tumeufanya kati ya Tume ya TEHAMA na wizara yetu, kwa sababu wizara yetu ndio inayosimamia mambo yote ya kidijitali kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa shindani na inakuwa katika viwango vya kidunia vya mambo hayo," alisema.

Aliongeza: "Tumefanya mambo mengi ambayo mmeyasikia, tumepeleka mawasiliano sehemu mbalimbali ikiwamo kujenga mkongo, sasa, tunaenda katika teknolojia ibukizi katika hizo, teknolojia ambayo ina jina kubwa sana ni akili mnemba na mambo ya roboti kama mnavyoona," alisema.

Alibainisha kuwa tume ina mpango wa kununua maroboti mengine ambayo watakuwa wanafanya kazi na vyuo mbalimbali na watu wengine.

"Kazi kubwa ni kukuza ubunifu wa kidijitali na maroboti kama haya yana matumizi mengi ya kijamii, tulichokifanya hapa, tumemleta huyu roboti na roboti kama mnavyofahamu anaitwa Eunice na yeye amewekewa teknolojia za kisasa sana, anaweza kuona na anaweza kusikia na anaweza kufanya mazungumzo na watu," alisema.

Alisema jukumu lao kwa sasa ni kutambua roboti zipi zitatumika maeneo ya viwandani, ni roboti zipi ambazo zinatumika katika maeneo ya super market, roboti zipi zinatumika katika maeneo ya ajali.

Aliongeza: "Lakini, ninataka kuwatoa wasiwasi watu kuhusu kupoteza kazi, siyo kweli. Roboti zitatufanya shughuli zetu kwa tija zaidi kwa mfano kama ulikuwa unafanya uzalishaji kwa wiki moja sasa hivi unaweza kufanya kwa muda mfupi zaidi".

## Wagonjwa 2,687 wapata huduma za kibingwa siku 7

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MADAKTARI bingwa wametoa huduma za matibabu ya kibingwa na kibobezi kwa wananchi zaidi ya 2,687 wa Mkoa wa Singida katika kambi maalum ya siku saba.

Madaktari hao 40 walitoa huduma hizo kwa wananchi katika kipindi cha siku saba ambacho waliweka kambi mkoani Singida kwenye hospitali zote za wilaya mkoani hapa.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk.Victorina Ludovick, akizungumza jana wakati madaktari hao wakitoa ripoti kwa kila wilaya walichobaini, alisema pia katika kipindi hicho wagonjwa 69 wamefanyiwa upasuaji.

Alisema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano wa viongozi wa mkoa ngazi zote na kwamba dawa na vifaa tiba vilikuwapo vya kutosha katika hospitali zote wakati madaktari hao wanatoa huduma kwa wananchi.

Dk. Ludovick alisema mafanikio mengine ni kuongezeka kwa mapato kwenye hospitali ambazo madaktari hao walikuwa wakitoa huduma kutokana na kuwepo kwa wagonjwa wengi.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa Singida, Dk. Fatuma Mganga, aliwapongeza na kuwashukuru madaktari hao kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa siku hizo.

Alisema ujio wa madaktari hao mkoani Singida pamoja na kutoa matibabu kwa wananchi kumesaidia kutoa elimu kwa watalaamu wa afya wa kada mbalimbali hali ambayo itasaidia kuimarisha utoaji wa huduma za kiafya kwa wananchi wa Mkoa wa Singida.

Kuhusu tatizo la upungufu wa wataalamu katika sekta ya afya, alisema Serikali ya Mkoa wa Singida imejipanga vizuri ili kuhakikisha tatizo hilo linapatiwa ufumbuzi haraka, ili wananchi waweze kupata huduma zote muhimu kwenye hospitali na vituo vya afya karibu na maeneo yao.

Baadhi ya madaktari bingwa na bobezi waliokuwa wanatoa matibabu kwa wananchi mkoani humo waliipongeza serikali kwa kuanzisha mkakati maalum kwa madaktari bingwa kwenda maeneo mbalimbali nchini kutoa matibabu kwa wananchi.





# Usimamizi hafifu wakwamisha mradi wa bil.99/- kukamilika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTEKELEZAJI wa mradi wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira unaogharimu Sh. bilioni 99, unasuasua kutokana na usimamizi hafifu wa mkandarasi unaofanywa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA).

Hali hiyo ilibainika wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Maji, Kundo Mathew ambapo alibaini kuwa mkandarasi anayetekeleza mradi huo ametumia nusu ya muda wa mkataba lakini utekekelezaji umefikia asilimia 20 pekee.

Alisema mkandarasi huyo yuko nyuma ya muda wa mkataba na hivyo anahitaji usimamizi wa karibu ili akamilishe mradi kwa wakati na wananchi waanze kunufaika nao.

Aliwataka kama kunaibuka tatizo lolote la utekelezaji wa mradi huo kuwasilisha mapema wizarani ili waone namna ya kushirikiana na serikali ya mkoa kutatua.

"Sijaridhishwa hata kidogo na utekelezaji wa mradi huu, mkandarasi yuko nyuma ya muda kabisa, sasa nadhani hapa wote tunaelewana kuwa tupo nyuma ya muda kwahiyo hakikisheni mnamsimamia vizuri mkandarasi," alisema Mathew.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge alisema mradi huo ni wa kimkakati na una lengo la kutatua kero ya uhaba wa maji katika Jiji la Mbeya na baadhi ya wilaya za jirani.

Alisema kutokana na kusuasua kwa mradi huo, wanakusudia kuitisha kikao cha dharura na wataalamu wa Mbeya-WSSA ili kujua kwa kina sababu zinazofanya mradi huo kuendelea kusuasua na hatua zinazostahili kuchukuliwa.

Alisema wamekuwa wakiwaaminisha wananchi kwamba mradi huo utatatua kero ya maji na hivyo kitendo cha kuendelea kuchelewa kinasababisha wananchi kutoiamini serikali.

Msimamizi wa mradi huo, Anord Martin alisema zipo sababu mbalimbali ambazo zinasababisha kusuasua kwa mradi ikiwemo ubovu wa barabara inayoelekea kwenye eneo la chanzo hali ambayo inasababisha kushindwa kufikisha vifaa kwa wakati.


Vilevile, alisema kuna baadhi ya maeneo ambayo mradi unapita kwenye maeneo ya wananchi ambao wanahitaji kulipwa fidia lakini bado hawajalipwa.

Aliiomba serikali kuwasaidia kuondoa vikwazo, hivyo ili waendelee na kasi ya ujenzi na kukamilisha mradi kwa wakati uliopangwa kwenye mkataba akidai kuwa kwenye baadhi ya maeneo yakiwemo yanayomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) walishamalizana nao.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mbeya-WSSA, Edna Mwaigomole alisema watashirikiana na menejimenti ya mamlaka hiyo kutatua vikwazo vinavyosababisha mradi huo ukwame ikiwemo kulipa fidia wananchi wanaostahili.

Alisema kama itatokea kikwazo ambacho kitakuwa nje ya uwezo wao, watawasilisha wizarani kwa ajili ya kuomba msaada wa utatuzi.

Mradi huo utakapokamilika utahudumia Jiji la Mbeya na wilaya zingine zikiwemo Chunya, Mbozi na Mji wa Tunduma mkoani Songwe.



Mkurungenzi wa Mradi wa Afya Thabiti, unaotekelezwa na Shirika la Amref Tanzania, Dk. Edwin Kilimba (kushoto), akizungumza na baadhi ya wakuu wa idara Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), walipofika jijini Dodoma jana kwa ajili ya kuutambulisha mradi huo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# BBT yatua Njombe, yaleta neema kwa vijana

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WIZARA ya Kilimo imesema serikali imeanzisha mradi wa BBT kila halmashauri nchini ikiwemo wilayani Njombe, ili kuwasaidia vijana katika nyanja za kilimo pamoja na ujasiriamali.

Timu ya wataalamu toka Wizara ya Kilimo wakiongozwa na Mratibu wa BBT, Vumilia Zinkankuba wamefika katika Wilaya ya Njombe kushuhudia mpango wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Kissa Kasongwa kuanzisha programu ya fursa kwa vijana na kutembelea Amcos ya kilimo ya Isowelu Mtwango.

Zinkankuba alisema mpango wa Wilaya ya Njombe umewavutia na kuwalazimu kuanzia Njombe kwa ngazi za halmashauri ambako tayari kumeonesha mwanga, hivyo watakuwa bega kwa bega kuendeleza programu hiyo.

"Sisi Wizara ya Kilimo tuko tayari, tumekuja kujifunza na kuja kuona sehemu gani inatakiwa kuja kukwamuliwa, maana kama wizara tuna mtaji, kikubwa ni nyinyi kubainisha eneo na kusema tunalima kitu gani? pamoja na sehemu ya kusafirisha kama ni Kenya au wapi pamoja na maghala," alisema Zinkankuba.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa alisema kuna vijana zaidi ya 600 toka maeneo mbalimbali ambao wanatamani kufanya shughuli ya kilimo ili kukabiliana na changamoto ya kiuchumi na upungufu wa ajira nchini.

Mwenyekiti wa Isowelu Amcos, Elia Mhonjwa alisema utaratibu wa kuwakopesha pembejeo wanachama wao umesaidia mkulima kupata gunia 80 hadi 200 za viazi kwenye shamba la ekari moja.

Baada ya zaiara hiyo, vijana hao akiwemo, Jeni Mfikwa aliliambia Nipashe kuwa wanashauku kubwa ya kupata fursa hizo ambazo wanaamini zitawakwamua na changamoto za kimaisha.

# Nchimbi ataka maofisa utumishi kuacha uonevu

**Na Halfani Chusi**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi, Dk. Emmanuel Nchimbi amewataka watumishi wanaosimamia utawala na rasilimali watu sehemu za kazi kuwatendea haki wafanyakazi wote kwa kujiepusha na vitendo vyovyote vya uonevu.

Akizungumza kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wataalam wa Rasilimali Watu na Utawala Duniani, juzi ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Morogoro, aliwataka watumishi wanaosimamia rasilimali watu na utawala kujiepusha na uminyaji haki na kujali stahiki za wafanyakazi, zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Alikumbushia kuwa dhamana ya nafasi zao za kusimamia utawala na rasilimali watu zitaendelea kuhitajika na kuheshimika iwapo baadhi ya watendaji wanaoendekeza tabia ya kujifanya 'miungu watu', na kuweka mbele maslahi binafsi katika ofisi wanazozisimamia, wataacha tabia hizo.

Aidha, aliwataka wanachama wa Chama cha Wataalamu wa Rasilimali Watu na Utawala Tanzania (THRAPA), kila mmoja wao kujiona ana deni la kutoa utumishi wa kusaidia wafanyakazi kupata haki na maslahi yao katika sehemu zao za kazi.

Alimwelekeza Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kukutana na uongozi wa THRAPA, ili kumaliza hali hiyo inayowakabili wataalamu wa utawala na rasilimali watu walioko katika sekta ya umma, ambao wamekuwa wakizuiwa na baadhi ya waajiri wao kushiriki shughuli au kuwa wanachama wa THRAPA.

Katika hatua nyingine, Balozi Nchimbi alikubali ombi la wanachama wa THRAPA waliomtaka awe mlezi wao, huku pia akiunga mkono dhamira yao ya kutaka chama hicho kiwe na bodi ya kitaaluma kama zilivyo bodi za baadhi ya taaluma nyingine na kusisitiza kuwa katika jambo hilo CCM itakuwa nao bega kwa bega kulifanikisha.



## Makamu wa Rais ahimiza uzalishaji chumvi kitaalamu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema wazalishaji wa chumvi katika Kijiji cha Shengejuu Wilaya ya Wete Pemba wanafursa ya kujikwamua na umasikini iwapo watasaidiwa kuzalisha kitaalamu.

Aliyasema hayo jana alipotembelea mashamba ya ushirika wa wazalishaji chumvi wa Kijiji cha Shengejuu kisiwani hapa, kuona changamoto zilizopo kwenye eneo hilo zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi na vitendo vya binaadamu vinavyosababisha uharibifu wa mazingira.

Alisema eneo hilo ni muhimu na limechukuwa idadi kuwa ya wananchi waliojiajiri, lakini mbali ya kuwa na changamoto ya miundombinu suala la mabadiliko ya tabia nchi nalo limeathiri uzalishaji wa chumvi katika eneo hilo na kupungunza matumaini ya wazalishaji hao.

Aidha, alisema kutokana na hali hiyo serikali itapeleka wataalamu wake kwenda kuona na kufanya tathimini ili kuja na mpango sahihi wa kusaidia kunusuru hali katika eneo hilo na wazalishaji waweze kuendelea na shughuli zao ikiwa ni pamoja na kuibua fursa zaidi kwenye eneo hilo.

Hivi sasa katika eneo hilo lenye idadi kubwa ya wajasiriamali wanaozalisha chumvi, kingo za mashamba yanayotumika kuzalisha chumvi zimeharibika.

Othman alisema hatua ya kupeleka wataalamu itasaidia kufanya tathimini ili kuja na mikakati bora na kuandaliwa mpango madhubuti utakaotumika kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na matendo ya wanaadamu ndani ya eneo hilo.

Alisem tatizo la tabia nchi ni la kidunia, kwamba sehemu kubwa ya hali hiyo inatokana na nchi tajiri zenye viwanda vikubwa duniani na shughuli zao za uzalishaji viwandani kuongeza joto duniani.

Alisema hali hiyo imechangia sana barafu iliyopo katika sehemu tofauti kuyayuka na kusababisha kina cha maji kuongezeka, lwaathirika wakubwa ni nchi masikini ikiwemo Zanzibar.

Othman alisema hivi sasa serikali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuirejesha Zanzibar kuwa ya kijani na kwamba wananchi hao pia watapewa fursa ya kushiriki katika suala la upandaji miti pamoja na kuanzisha vitalu vya miti.

Mkuu wa Wilaya ya Wete, Dk. Hamad Omar Bakari alisema pamoja na kuwepo changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi lakini matendo ya binaadamu nayo yamechangia katika uharibifu wa maeneo.

Alisema kuna haja ya wananchi kubadilika hasa katika suala la ukataji wa miti ovyo, kutokana na ukweli kwamba matendo ya namna hiyo ndiyo chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira.

Baadhi wa wakulimwa wa chumvi katika eneo hilo walisema licha ya jitihada kubwa wanazofanya kujenga matuta ya kuzuia maji hayo yasiathiri mashamba yao, lakini kutokana na nguvu kubwa ya maji inayoongezeka kila siku uzalishaji huo umeshuka.

# W'biashara 156 wakamatwa na mifuko ya plastiki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA 156 wamekamatwa wakituhumiwa kuingiza mifuko ya plastiki visiwani Zanzibar.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kikwajuni, Nassor Salim Ali, aliyetaka kujua mikakati ya serikali katika kudhibiti uingizaji wa mifuko ya plastiki imefikia wapi.

Akijibu swali hilo, Haruni alisema kupitia Mamalaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) imeanzisha kikosi maalumu kinachofanya operesheni za kusaka mifuko ya plastiki ikiwemo wafanyabiashara wanaoingiza mifuko hiyo.

Alisema watu 156 wamekamatwa katika operesheni 80 zilizofanywa, kwamba kilo 481 za mifuko hiyo zimekamatwa.

Akifafanua zaidi alisema baadhi ya watu waliokamatwa wamepigwa faini, kwamba serikali imepata Sh.milioni 17,770 kutokana na faini izo.

Haruni alisema imebainika baadhi ya maeneo ambayo yanaingiza mifuko ya plastiki kwa wingi ni kupitia katika bandari ambazo sio rasmi zilizopo Unguja na Pemba.

Aidha, alisema Zanzibar zipo Bandari nyingi ambazo sio rasmi ambazo zote zinatumika kuingiza vitu au bidhaa kinyume na sheria ikiwemo mifuko ya plastiki.

Alisema: "Wafanyabiashara na watu wengine wanafahamu vizuri kuhusu mifuko ya plastiki ambayo imepigwa marufuku kwa sasa na ndiyo maana wanatumia vituo ambavyo sio rasmi kuingiza bidhaa hizo".

Hata hivyo alisema serikali ipo katika mikakati ikiwemo kutafuta wawekezaji kwa ajili ya mpango wa uchakataji na usarifu wa taka kwa matumizi mbalimbali ikiwemo mbolea kwa wakulima.




Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Marzui, akizungumza katika hafla ya utiaji saini mkataba wa manunuzi ya vifaa tiba kati ya wizara hiyo na UNICEF kupitia mradi wa uwekezaji wa huduma ya mama na mtoto (TMCHIP), wenye thamani ya dola za kimarekani 12,500,000, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ, UNICEF zakubaliana ununuzi vifaa tiba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) zimeingia makubaliano ya mkataba wa manunuzi wa vifaa tiba wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 12.5 kupitia utekelezaji wa mradi wa uwekezaji huduma ya mama na mtoto.

Akizungumza baada ya hafla hiyo ya utiaji saini uliofanyika visiwani Zanzibar, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema mpango huo ni safari ya mabadiliko inayolenga kuunda mfumo thabiti wa utoaji wa huduma za afya.

Alisema miongoni mwa malengo ya mradi huo ni kuboresha utoaji wa huduma bora za uzazi na huduma za mtoto na wamedhamiria kuinua viwango vya utunzaji katika kila ngazi, kuhakikisha kuwa kila mama na mtoto wanapata huduma bora za afya.

Alisema lengo lingine ni kuboresha upatikanaji na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika huduma za afya na ushirikiano wa teknolojia ya mawasiliano katika huduma za afya.

Alisema pia utaboresha usimamizi wa rekodi za wagonjwa na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma.

Alisema katika kukuza huduma za afya ya uzazi kwa vijana, serikali inakusudia kufanya huduma za afya ya uzazi zipatikane zaidi kwa vijana, katika vituo vya afya na ndani ya jamii.

"Kuboresha ushiriki wa jamii na ushiriki katika utoaji wa huduma za afya. Ushiriki wa jamii ni muhimu kwa mafanikio ya mpango wowote wa afya, tutafanya kazi ili kuhusisha na kuwezesha jamii kuchukua jukumu la kazi katika afya na ustawi wao" alisema.

Aidha, alisema katika makubaliano yao UNICEF itasaidia utoaji wa dawa muhimu na bidhaa za lishe, vifaa vya matibabu kwa ajili ya vituo vya afya vilivyokarabatiwa, magari kwa idara ya huduma za kuzuia na timu ya uratibu wa mradi, pamoja na vifaa.

Mwakilishi mkazi wa UNICEF, Elke Wisch alisema: "UNICEF inashukuru kwa kuendelea kutoa msaada kutoka Benki ya Dunia (WB) katika kuimarisha mfumo wa ikolojia ya afya ya kidijitali Zanzibar na imedhamiria kuendeleza ushirikiano huo".

Alisema ushirikiano huo unaashiria dhamira ya washirika wote katika kutanguliza ustawi wa wanawake na watoto, kuweka msingi wa mustakabali bora kwa Zanzibar.

Aidha, alisema miongoni mwa mafanikio muhimu ya ushirikiano katika afya ya kidijitali kati ya Serikali ya Zanzibar na UNICEF ni kubuni na kuendeleza maoni ya mteja, inayojulikana kama Zan Afya Maoni na kubuni na maendeleo ya zana ya usimamizi wa digitali kwa wafanyakazi wa afya.

Hata hivyo, alisema: "UNICEF inafurahi kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na juhudi za WB katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya na kuongeza uzoefu wa wagonjwa katika vituo vya afya".

Alisema UNICEF pia imelazimika kutoa msaada katika uwezo wa ununuzi ndani ya Wizara ya Afya, hasa katika matibabu ili kuboresha michakato ya ununuzi kwa utoaji bora wa huduma.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**NIKUSWIGA ISAKWISA MALAMBUGI** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne (form four) chenye majina ya **Luka J.Nebas** na namba za usajili **P.2378/0040,** kutoka shule ya **Airport Secondary School** Mwaka 2020 Mkoa wa mbeya. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **PHQ/TAN/KIL/4672/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**ANNA PETER KIJAZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya **BAJAJI** yenye usajiri wa **MC 548 BBZ.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu nae.

TAARIFA YA POLISI
**PHQ/TAN/KOR/4643/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDULRAHMAN AMOUR KHAMIS** anatangaza kupotea kwa kadi za magari zenye namba za usajili **T735 BRE, T 815 BTB, T 455 BJR, T179 BWW, T922 BZA, T261 CNB, T 416 DBE, T 316 CNB.** Kwa yeyote atakaezione atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/UBU/91871/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HASHIMU ABDALLAH MATAMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina yenye namba ya usajili **T350 DKH.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/UBU/90265/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AGNESS H. MINNJA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRY** yenye usajili namba **T204 CEY,** CHASSIS NUMBER: **DD51T363754** na ENGINE NUMBER: **F6AEAA3754.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA :
**PHQ/ARU/ARU/16162/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALAPIA SEHEWA LUNGWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S1207/0030** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAKUTOPORA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018, Cheti hiki kimepotea Jijini Dodoma. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/19094/2024**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO CHA JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 10984 YA MWAKA 2024.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU CLAVER RWEYEMAMU TEMALILWA**

**DOMINA ANCILLA KOKWIGANA TEMALILWA.....MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kusuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 19 mwezi wa 06 , 2024 saa 09:30 Asubuhi. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. Jaji A.A Omari.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 16 mwezi wa Mei, 2024.

HIGH COURT OF TANZANIA
NAIBU MSAJILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.20/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU STEVEN STEVEN KOLIMBA wa MBWANGA DODOMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA YOHANA STEVEN KOLIMBA**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 Mwezi 06 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 21 Mwezi 05 Mwaka 2024.

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.19/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SITUMAI F. KHERI wa BAHI ROAD**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JAWARA ADAMU CHORA**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 06 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 17 Mwezi 05 Mwaka 2024.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 11501/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late ESTER EXSAUD MAHENGE of Kikombo Within Dodoma City.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MAGDALENA EXSAUD MAHENGE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner
Objections to the grant should be filed on or before the 26th Day of JUNE, 2024
Dated at Dodoma this **20th Day of MAY , 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...14/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: STEPHEN PAUL HASHIM wa MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA STANLEY STEPHEN HASHIM**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi JUNI Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 15 mwezi 5 mwaka 2024

HAKIMU

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUS-TRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Aliyekuwa Rais wa Iran Raisi kuzikwa leo

## • Kaimu rais asema hakuna kitakachoharibika




Rais wa mpito wa Iran Mohammad Mokhber, akiongoza kikao cha baraza la mawaziri, jana.

**Na Maulid Mmbaga**

ALIYEKUWA Rais wa Iran Ebrahim Raisi na wengine nane waliopata ajali ya helikopta juzi wanatarajia kuzikwa leo katika mji wa Tabriz alikokuwa akisafiri, na kwamba miili yao itapelekwa kwanza kwenye idara ya uchunguzi wa kitaalamu kabla ya maziko.

Kiongozi mkuu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei alisema jana kuwa kutakuwa na maombolezo ya kitaifa ya siku tano kwa lengo la kutoa heshima ya mwisho kwa hayati Rais Raisi.

Wakati huo huo Baraza la mawaziri nchini humo lilimteua Naibu Waziri wa Mambo ya Nje Ali Bagheri Kani kuwa kaimu waziri wa mambo ya nje, baada ya kifo cha Hossein Abdollahian aliyekuwa waziri katika wizara hiyo.

Aidha, baada ya ajali hiyo maelezo zaidi yameanza kujitokeza yakieleza kilichotokea kwa mmoja wa abiria waliokuwemo ndani ya helikopta hiyo Mohammad Ali Al-Hashem, aliyekuwa Imamu wa Swala ya Ijumaa wa Tabriz, mji ambao msafara huo ulikuwa unaelekea.

Kwa mujibu wa Mohammad Nami, Mkuu wa Shirika la Kudhibiti Migogoro ya Iran, Al-Hashem alinusurika kwa saa nzima baada ya ajali hiyo ambayo iliuwa watu wote tisa waliokuwa ndani ya helikopta. Na kwamba imam alijaribu hata kuwasiliana na ofisi ya rais bila mafanikio.

"Hakuna uchunguzi wa chembechembe za vinasaba, DNA iliyohitajika kubaini abiria," Nami aliiambia BBC.

Ilielezwa kuwa Iran imeanza siku tano za maombolezo huku wananchi wakiandamana barabarani katika miji tofauti kote nchini humo, na kwamba mwili wa Rais Raisi utapelekwa kaskazini mashariki kuagwa, kasha kizikwa Mashhad kwenye kaburi la Imam Reza, mrithi wa nane wa Mtume Muhammad.

### HAKIHARIBIKI KITU

Baada ya Kiongozi wa juu wa kisiasa na kidini wa Iran Ayatollah Ali Khamenei kumtangaza kuwa kaimu Rais, Mohammad Mokhber aliongoza kikao cha kwanza cha baraza la mawaziri. Akiwahakikishia raia wa taifa hilo kuwa hakuna kitakachoharibika baada ya kifo cha Ebrahim Raisi.

Akizungumza katika televisheni ya taifa hilo Kaimu Rais Mokhber, alisema kwamba watafuata njia ya Rais Raisi katika kutekeleza majukumu waliyopewa bila usumbufu wowote.

"Hili ni tukio zito la kusikitisha kwetu sote. Linasababisha huzuni na uchungu lakini kuhusu suala la utawala na mwenendo wa nchi, watu wote wanapaswa kuwa na uhakika kuwa hakutakuwa na tatizo lolote," alisema Mokhber.

Hata hivyo, alisema nchi hiyo itaendelea kusonga mbele chini ya uongozi wake na kwamba kila mmoja anapaswa kuendelea na majukumu yake licha ya msiba huo. Akieleza kuwa kwa namna yoyote ile, kilichotokea hakipaswi kuingiliana na serikali na uendeshaji wa taifa la Iran.



Wananchi Iran wakiandamana barabarani ishara ya maombolezo baada ya kifo cha Rais Ebrahim Raisi, Waziri wa Mambo ya Nje na viongozi wengine, jana. **PICHA ZOTE MTANDAO.**

Kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo Mokhber, atahudumu katika nafasi ya kaimu rais wa Iran kwa kipindi cha siku 50 kabla ya kufanyika kwa uchaguzi maalumu Juni 28, mwaka huu.

Ilieleza kuwa mchakato wa uchaguzi wa mrithi wa Rais Raisi utaanza na fomu zitawasilishwa kati ya Mei 30 na Juni 3, mwaka huu, na kwamba orodha ya wagombea walioidhinishwa inatarajiwa kuchapishwa Juni 11 na uchaguzi utafanyika Juni 28.

Hapo litajulikana jina la mrithi wa hayati Rais Raisi, pia ni ishara ya shauku ya walio madarakani kuonesha kuwa licha ya kifo cha kiongozi huyo, hakuna mgogoro wa kisiasa au kitaasisi unaoripotiwa.

### KUHUSU HELIKOPTA

Wakati maelezo yakiendelea kujitokeza, vyombo vya habari vya serikali ya Iran vilisema kwamba helikopta iliyombeba rais na waziri wa mambo ya nje ilikuwa aina ya Bell 212.

Vilevile, ilielezwa kuwa haijulikani helikopta hiyo ilikuwa imefanya kazi kwa muda gani, lakini aina hiyo ya helikopta iliitengenezwa kwa jeshi la Canada miaka ya 1960. Huku ikielezwa kwamba miongo kadhaa ya vikwazo vya Marekani na kimataifa vilianza baada ya mapinduzi ya Iran mwaka 1979.

Ilibainishwa kuwa helikopta hizo zilitengenezwa na kampuni ya 'Bell Helicopter' ya Marekani na kutumika sana na waendeshaji wa serikali, ikiwa ni pamoja na vyombo vya sheria vya Marekani na polisi wa kitaifa wa Thailand.

Ilielezwa kuwa Jeshi la Wanamaji na la anga la Iran lina jumla ya helikopta hizo 10, kwa mujibu wa nyaraka ya 2024 ya Jeshi la Anga la Dunia la 'FlightGlobal', lakini haijulikani ni ngapi zinatumiwa na serikali ya Iran hadi sasa. Na kwamba zinaweza kutumiwa kufanya mambo tofauti kama kubeba watu na mizigo, na zinaweza kuwekwa silaha kwa ajili ya kupigana.

Shirika la habari la serikali la IRNA linasema kuwa helikopta iliyombeba rais inaweza kubeba abiria sita na wafanyakazi wawili.

Kwa mujibu wa Wakfu wa Usalama wa Ndege, shirika lisilo la kiserekali, ajali ya hivi karibuni iliyohusisha ndege aina ya Bell 212 ilitokea Septemba 2023 wakati mwanamitindo aliyekuwa akiendeshwa kwa faragha ilianguka kwenye ufuo wa Falme za Kiarabu. Na nyingine ilitokea Aprili 2018, wakati Bell 212 ikiwa inamsafirisha mgonjwa aliyekumbwa na mshtuko wa moyo.

***Chanzo mashirika ya kimataifa.***

# HATIMA YA MAKATA, TEGETE PAMBA FC KUJULIKANA JULAI

**Na Saada Akida**

HATIMA ya Kocha Mkuu wa Pamba Jiji FC, Mbwana Makata na mshambuliaji wa timu hiyo, Jerry Tegete, kubakia ndani ya kikosi hicho iko mashakani, imeelezwa.

Pamba Jiji FC itashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Ligi ya Championship msimu huu.

Bingwa wa Ligi ya Championship, Ken-Gold ya Mbeya pia imepanda daraja moja kwa moja huku timu nyingine mbili zitajulikana baada ya kumalizika kwa michezo ya mtoano.

Makata ameiwezesha Pamba Jiji FC kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya miaka 23 Pamba Jiji FC imerejea Ligi Kuu msimu huu na kunamfanya kocha Makata kuweka rekodi ya kuwa kocha pekee Tanzania ambaye amezipandisha daraja timu nne ndani ya misimu saba.

Kocha huyo pia aliwahi kuipandisha Alliance FC msimu katika mwaka 2017/18, Polisi Tanzania 2018/19, Dodoma Jiji 2019/20 huku Jerry Tegete, akiwa mmoja wa nyota walioipandisha timu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Pamba Jiji, Martin Sawema, alisema Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo itakutana kati ya Juni mwishoni au mapema Julai ili kujadili na kuweka mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuelekea msimu ujao.

"Hatutaki kuwa katika historia ya kupanda na msimu unaofuata kushuka, tunahitaji kufanya maboresho makubwa ndani ya kikosi ikiwamo usajili mzuri na kuangalia uwezekano wa kubakia na Kocha Makata.

Aliongeza kikao hicho kinatarajia pia kupokea ripoti ya kocha kuhusu mapendekezo ya nyota watakaosajiliwa kwa ajili ya msimu mpya kwa sababu wanataka kumaliza katika nafasi nne za juu.

"Kama tunahitaji kumaliza katika nafasi nne za juu na kutoshuka daraja, lazima tuimarishe kikosi, na kawaida kwa timu zinazopanda daraja kucheza Ligi Kuu zinatakiwa kufanya usajili mkubwa kwa kupunguza baadhi ya wachezaji waliopandisha na kuleta wengine," Sawema alisema.




Ofisa Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha (katikati) akiwa na Mkuu wa Masoko wa Parimatch, Levis Paul (kushoto) na Meneja Mkuu wa Hisense Tanzania, Tahera Karim, wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya michuano ya Ulaya 'Euro 2024' itakayofanyika hivi karibuni nchini Ujerumani. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mashabiki kushuhudia live mashindano ya Euro 2024

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI michuano ya Mataifa ya Ulaya 'Euro 2024' ikitarajiwa kufanyika kuanzia Juni 14 hadi Julai 14, mwaka huu, mashabiki wa soka nchini wametakiwa kuchangamkia fursa za kwenda kutazama mechi za michuano hiyo.

Euro 2024 imepangwa kufanyika katika miji ya Berlin, Munich, Frankfurt na Hamburg nchini Ujerumani na nchi 24 zinatarajiwa kushiriki fainali hizo za mwaka huu.

Katika kufanikisha mashabiki wa soka wanapata fursa ya kushiriki fainali hizo, Kampuni za Tigo, Hisense na Parimatch wameandaa kampeni ya kuwezesha baadhi ya mashabiki kwenda kutazama baadhi ya mechi za michuano hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha, alisema michuano ya 'Euro' si tu tukio la kimichezo bali ni jambo la kimataifa ambalo linaunganisha mamilioni ya mashabiki wa soka duniani kote.

"Nchini Tanzania soka lina nafasi ya pekee katika mioyo ya wengi, tuliona hii ni fursa muhimu sana ya kuwasogeza mashabiki karibu na michuano hiyo kupitia kampeni yetu ya 'Zigo la Euro Cup na Hisense', kupitia kampeni hii mashabiki ambao ni wateja wetu wanawaweza kushiriki kwa kufanya malipo ya bili kupitia Tigo Pesa Super App," alisema Angelica.

Naye Meneja wa Hisense Tanzania, Tahera Karim, alisema wamejitolea kuongeza teknolojia bora zaidi ya burudani kwa mashabiki wa soka kupitia kampeni hiyo.

Alisema mashabiki wa soka watapata fursa ya kwenda kushuhudia baadhi ya mechi ya michuano hiyo kwa kuweka ubashiri wa michezo mbalimbali kutumia Parimatch kupitia huduma ya Tigopesa kwenye 'Super App'.

# Tanzania yang'ara michuano CAF U-15

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wavulana wa umri chini ya miaka 15 imeanza vyema katika mashindano ya mashule Afrika baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Morocco katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan Complex jana asubuhi.

Bao pekee la wenyeji hao lilifungwa na mchezaji wa Morocco, aliyekuwa katika harakati za kuokoa hatari kwenye lango lao huku ikitoka suluhu dhidi ya Senegal katika mechi yake ya pili.

Kwa upande wa wasichana, Tanzania iliendelea kung'ara baada ya kuwafunga yosso wenzao kutoka Morocco bao 1-0 huku Afrika ya Kusini wavulana wakishinda mabao 3-0 dhidi ya Libya huku Afrika Kusini wasichana wakitoka sare ya bao 1-1 na Uganda.

Guinea wavulana wamepata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Benin, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex.

Mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), yanaendelea tena leo na mshindi kwa kila upande atapata zawadi ya Dola za Marekani 300,000 ambazo zitaelekezwa kwenye mpango wa maendeleo.

## Tabora United FC 'vita' muhimu Bara

**Na Adam Fungamwango**

KAMA haitaki kushuka daraja au kucheza mechi ya mchujo, 'play off', Tabora United inahitaji kupata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mkoani Tabora.

Katika msimamo, Tabora United ipo nafasi ya 14, eneo la hatari, ikiwa na pointi 26, hivyo inahitaji pointi tatu ili kufufua matumaini ya kubakia kwenye ligi hiyo.

Kocha Msaidizi wa Tabora United, Benard Fabian, amekiri mechi ya leo ni kusuka au kunyoa, kwa sababu wanachohitaji ni matokeo ya ushindi na si vinginevyo ili kujiepusha kurudi walikotoka msimu uliopita.

"Maandalizi yetu yanakwenda vizuri, tunajua uhitaji wa huo mchezo, ni mechi muhimu kwetu kama tunataka kusalia Ligi Kuu basi inapaswa kushinda mechi hiyo, kwetu ni fainali," alisema kocha huyo.

Naye Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala, amesisitiza 'Wana-Tabora' hawapo tayari kuiona timu yao inateremka daraja ndani ya 'mikono' yao huku mechi yao inayofuata ikiwa ni dhidi ya dhidi ya Yanga itakayochezwa Jumamosi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KOMPANY ATAJWA BAYERN
KOCHA wa Burnley, Vincent Kompany, mwenye umri wa miaka 38 ni miongoni mwa walimu wanaopigiwa upatu kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel huko Bayern Munich. ***(Fabrizio Romano)***

### BARKLEY KIMEELEWEKA VILLA
KLABU ya Aston Villa inakaribia kufikia makubaliano ya kumnunua tena mchezaji wa Luton Town na kiungo wa kati wa zamani wa England, Ross Barkley kwa mkataba wa kudumu, miaka minne baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kujiunga kwa mkopo kutoka Chelsea. ***(Guardian)***

### ISAK, BROBBEY KUTUA ARSENAL
ARSENAL inataka kusajili mshambuliaji kabla ya ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya, huku nyota wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak, mwenye umri wa miaka 24 na mshambuliaji wa Ajax na Uholanzi, Brian Brobbey, wakiongoza orodha hiyo. ***(Independent)***

### MCKENNA AGEUKA LULU
CHELSEA na Manchester United zote zimewasiliana na Kocha wa Ipswich Town, Kieran McKenna, huku raia huyo wa Ireland Kaskazini akiwa katika harakati za kuchukua nafasi ya Mauricio Pochettino au Erik ten Hag. ***(Manchester Evening News)***

### NETO KUITAJIRISHA WOLVES
KLABU ya Wolves itadai kulipwa pauni milioni 60, kiasi ambacho kitavunja rekodi ya klabu endapo itamuuza winga wake raia wa Ureno mwenye umri wa miaka 24, Pedro Neto, ambaye analengwa na Manchester City na Newcastle United msimu wa joto. ***(Telegraph )***

### VILLA KUMUUZA CARLOS
KLABU ya Aston Villa iko tayari kusikiliza ofa kwa mlinzi wa Brazil, Diego Carlos mwenye umri wa miaka 31. ***(Telegraph)***

### EMERY AMTAKA ARAUJO
KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery, anataka kumsajili beki wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uruguay, Ronald Araujo mwenye umri wa miaka 25. ***(Sport)***

### COADY ANUKIA STOKE CITY
KLABU ya Stoke City imeonyesha nia ya kutaka kumsajili beki, Conor Coady, mwenye umri wA miaka 31 kutoka Leicester***(Teamtalk)***,

### KONATE SOKONI ENGLAND
KLABU ya Leicester inajiandaa kushindana na Lyon na Brest zote za Ufaransa katika mchakato wa kumnunua fowadi wa Burkina Faso, Mohamed Konate, mwenye umri wa miaka 26, ambaye mkataba wake na Akhmat Grozny ya Urusi unamalizika msimu huu. ***(Football Insider)***

### SPURS KUSAJILI WATATU
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, ameiomba klabu hiyo kusajili wachezaji watatu wapya kwa ajili ya msimu mpya. ***(ESPN)***

### BRANTHWAITE KUTUA UNITED
MANCHESTER United inavutiwa na mlinzi wa Everton, Jarrad Branthwaite, mwenye umri wa miaka 21, na The Toffees wanaweza kumnunua beki wa kati wa Galatasaray na Colombia, Davinson Sanchez (27), kuziba nafasi ya nyota huyo anayewindwa.***(Caught Offside)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RAYA: NINATAKA KUBAKI ARSENAL

**Kipa huyo asema 'ndoto' yake itatimia endapo Mikel...**

**LONDON, England**

DAVID Raya amekiri kuwa "ndoto itatimia" ikiwa Arsenal watamsajili kwa mkataba wa kudumu msimu huu wa kiangazi huku mkopo wake kutoka Brentford ukikaribia mwisho.

Akiwa amecheza mechi 16 bila kuruhusu bao, jambo ambalo limemfanya achukue tuzo ya Golden Glove, Raya amekuwa na mchango mkubwa katika kikosi cha Arsenal ambao wamemaliza katika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu England.

Mkopo wa Raya kutoka Brentford unajumuisha kipengele cha ununuzi ambacho alikiri anatumaini kitafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.

Katika mahojiano na Daily Mail, Mhispania huyo alikiri: „Bila shaka, ningependa kuwa hapa msimu ujao. Itakuwa ajabu, ndoto kutimia kusaini klabu hii.

"Si juu yangu. Ni juu ya klabu na Mikel. Ikiwa uchezaji wangu umekuwa mzuri vya kutosha basi natumaini watanipa mkataba wa muda mrefu."

Arsenal wanatarajiwa kuanzisha kipengele chao cha kumnunua Raya, hatua ambayo huenda ikamaliza muda wa Aaron Ramsdale katika klabu hiyo.

Ramsdale alipoteza nafasi yake kuelekea mwanzo wa msimu na anahitimisha kampeni akiwa na mechi 11 pekee katika mashindano yote.

Huku msimu mwingine ukikaribia ukingoni, Ramsdale anatarajiwa kuzingatia chaguzi zake mwaka huu na ameivutia Newcastle United, ingawa kipa huyo aliingia katika mitandao ya kijamii kusisitiza ripoti za makubaliano hazijafikiwa.

# MO SALAH ATOA LA MOYONI LIVERPOOL

**LIBERPOOL, England**

MOHAMED Salah ametoa kauli kali kuhusu mustakabali wake ndani ya Liverpool kwa kusema „nitapigana kama kuzimu" kushinda mataji kwa klabu hiyo msimu ujao.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri mwenye umri wa miaka 31, anaingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Liverpool mwezi ujao, kukiwa hakuna makubaliano ambayo yamefikiwa kati ya klabu na Salah, kuhusu kuongeza muda wake wa kukaa Anfield.

Liverpool ilikataa ofa ya pauni milioni 150 kutoka kwa Al Ittihad ya Saudi Arabia kwa ajili ya Salah katika siku za mwisho za dirisha la usajili la majira ya kiangazi yaliyopita, lakini dau jipya kutoka kwa Saudi Pro League la kutaka kumsajili Salah linatarajiwa wakati wa dirisha lijalo la uhamisho.

Huku Jurgen Klopp akiachia ngazi kama kocha mwishoni msimu baada ya kuhudumu kwa miaka nane na nusu, na Kocha wa Feyenoord, Arne Slot, alithibitisha kuwa mrithi wake kwa mkataba wa miaka mitatu.

Katika chapisho kwenye mtandao wa kijamii, Salah amedokeza Liverpool msimu ujao baada ya kusema anataka kuleta mafanikio zaidi kwa klabu hiyo.

„Tunajua mataji ndiyo yana umuhimu na tutafanya kila tuwezalo kufanikisha hilo msimu ujao," alisema Salah.

„Mashabiki wetu wanastahili na tutapigana kama kuzimu."

Salah pia alimsifu kocha anayeondoka, ambaye aligombana naye kwenye mstari wakati wa mchezo dhidi ya West Ham United.

„Ilikuwa nzuri kushiriki nawe mataji hayo yote na uzoefu katika kipindi cha miaka saba iliyopita," Salah alisema pamoja na picha yake na Klopp. „Nakutakia mafanikio mema kwa siku zijazo na natumai tutakutana tena."

Meneja mpya, Slot, ataiongoza Liverpool rasmi kuanzia Juni Mosi, mwaka huu huku mchezo wake wa kwanza ukipangwa kuwa wa kirafiki wa kujiandaa na msimu ujao dhidi ya Real Betis utakaochezwa Julai 26, huko mjini Pittsburgh.

Kwa kuwa Salah hatashiriki katika michuano mikubwa ya kimataifa msimu huu wa joto, huenda akahusika katika mchezo wa kwanza wa Slot, huku wachezaji wenzake wa Liverpool walioshiriki michuano ya Copa America na Euro 2024 wakipata mapumziko majira ya kiangazi.




## Ange ataka watatu Spurs

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, ameiomba klabu hiyo kusajili angalau wachezaji watatu wapya katika dirisha la majira ya joto, vyanzo vimeiambia ESPN.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 58 anataka kuendeleza mabadiliko ya kikosi chake baada ya Spurs kumaliza katika nafasi ya tano katika msimu wake wa kwanza wa kuinoa timu hiyo na kukosa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa pointi mbili.

Vyanzo vya habari vinasema Postecoglou ana uhalisia kuhusu kiwango cha mabadiliko anachoweza kufikia katika dirisha moja lakini Tottenham wana nafasi ya kutosha ndani ya Kanuni za Faida na Uendelevu za Ligi Kuu England na kocha huyo wa Australia analenga mshambuliaji mpya na kiungo wa kati kati ya wachezaji wapya wanaoweza kuongezwa.

Haijulikani kwa wakati huu ni kina nani wanaolengwa na Spurs lakini vyanzo vimeiambia ESPN klabu hiyo ya London Kaskazini inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney na imekuwa ikimfuatilia kiungo wa Chelsea, Conor Gallagher, kwa miezi kadhaa.

Toney anatarajiwa kuondoka Brentford msimu huu wa joto, wakati Gallagher amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake Stamford Bridge na inasemekana pia anavutiwa na Aston Villa.

Mipango ya Postecoglou itaimarishwa na mauzo ya wachezaji wowote huku Spurs ikifikiriwa tayari kusikiliza ofa kwa idadi ya wachezaji wake akiwamo, Pierre-Emile Højbjerg, Giovani Lo Celso na Bryan Gil.



## Pochettino njia panda Chelsea

**LONDON, England**

MAURICIO Pochettino bado hana uhakika kama hatima yake itaendelea Chelsea, licha ya kukutana na mmiliki mwenza wa klabu hiyo, Todd Boehly.

The Blues walifanikiwa kupata ushindi dhidi ya Bournemouth katika siku ya mwisho ya kampeni na kujihakikishia nafasi ya kucheza Ulaya msimu ujao.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kupata ushindi mara tano mfululizo katika Ligi Kuu tangu Machi, mwaka 2022 na hivyo kumaliza msimu wao mgumu kwa kiwango cha juu.

Mafanikio yao, hata hivyo, hayajatosha kumweka Pochettino kuwa na raha kwa sababu bosi huyo raia wa Argentina bado hana uhakika na mustakabali wake.

„Sijui kuhusu hili. Ninachoweza kukwambia ni Ijumaa usiku, Todd Boehly alinialika kwa chakula cha jioni na ilikuwa chakula cha jioni kizuri sana pamoja.

„Lakini sijui kuhusu uvumi. Wafanyakazi wangu kesho (leo), wanasafiri kwa ndege kwa ajili ya likizo zao. Nitabaki London kwa siku chache zaidi. Simu yangu itawashwa."

Pochettino, ambaye atapata nafasi ya kutoa maoni yake kuhusu utendaji wa kazi wa klabu hiyo na pia kupokea mapitio ya utendaji wake.

Bosi huyo alipoombwa kueleza zaidi juu ya mkutano wake na Boehly, akajibu: „Sitaelezea. Ni kwa ajili yako tu kujua kwamba nilikuwa naye. Sitazungumza juu ya hili.

Pochettino alihakikisha anakamilisha kampeni, akiwashukuru wachezaji wake kwa kuendelea kupambana.

„Nimefurahishwa na kujivunia sana kuhusu wachezaji," alieleza. "Ungeweza kuona mwisho wa mchezo, wachezaji ambao walicheza zaidi chini na kuumia, jinsi walivyokuja kunikumbatia."



# TEMBO WARRIORS YATINGA ROBO FAINALI YA AAFCON

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Walemavu (Tembo Warriors), imetinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AAFCON) yanayoendelea nchini Misri baada ya kumfunga Sierra Leone mabao 2-0.

Tembo Warriors ilipata ushindi katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Al Salaam uliko jijini Cairo juzi usiku huku wachezaji wake wakionyesha kiwango bora wakati wote.

Wawakilishi hao wa Tanzania wako katika Kundi D, pamoja na Angola na Sierra Leone na jana usiku walitarajia kushuka dimbani kuvaana na Angola, na mechi hiyo ndio itatoa nafasi ya nani atakayeongoza kundi hilo.

Sierra Lione wameondolewa katika mashindano hayo baada ya kufungwa na Angola mabao 4-0 katika mechi ya kwanza.

Baada ya ushindi wa Tembo Warriors, timu hiyo imeendelea kunufaika na 'Goli la Mama', kwa kupata Sh. milioni 10, ikiwa ni hamasa ambapo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aliahidi kununua kila bao kwa dau la Sh. milioni tano.

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Suleiman Selela, ameshakabidhi fedha hizo kwa wachezaji na kuwaeleza ahadi ya Rais Samia iko pale pale.

Selela alisema kitendo cha kufanya vizuri katika mchezo wa kwanza kimemfurahisha Rais Samia ambaye anaendelea na ahadi yake ya kununua bao moja kwa Sh. milioni tano kwa kila wanaposhinda katika mashindano hayo.

"Mshinde mtakavyoweza, licha ya kuangalia goli la mama pia kufikia malengo yetu ya kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania na kuendelea kusonga mbele na kuvuka kibabe katika mashindano haya," alisema Selela.

Mashindano hayo yatatoa timu nne zitakazoiwakilisha Afrika katika fainali za Kombe la Dunia zitakazochezwa mwaka 2026.



Msanii wa muziki wa kizazi kipya, Dotto Bwakeya maarufu Lameck Ditto (kulia), akiwa katika Mahakama ya Kanda Kuu ya Dar es Salaam kwa ajili ya kusikiliza kesi yake ya madai dhidi ya Kampuni ya Multi Choice Tanzania (DSTV). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi wa DSTV aitaja wizara kesi madai Ditto

**Na Mwandishi Wetu**

SHAHIDI wa kwanza wa Multchoice Tanzania maarufu DSTV, Astrid Mapunda, ameitaja Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusika katika wimbo wa Nchi Yangu ambao msanii, Dotto Bwakeya (Lameck Ditto), anadai ni wake na kampuni hiyo iliutumia katika matangazo ya kibiashara bila idhini yake.

Mbele ya Jaji Mfawidhi, Salma Maghimbi, juzi shahidi huyo alipinga madai ya Ditto akiieleza mahakama mmiliki wa wimbo wa Nchi yangu siyo Ditto.

Alidai anafahamu wimbo wa Nchi Yangu ulioimbwa na Tanzania All Stars ulitumiwa na serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na ulizinduliwa wakati wa Tamasha la Urithi.

Katika ushahidi wake, Mapunda alidai mwaka wa 2018, wizara hiyo ilikuwa na kampeni ya uzalendo iliyopewa jina la Tamasha la Urithi.

"Kwenye tamasha hilo, wizara ilishirikiana na chombo cha habari cha Clouds Media Group chini ya uongozi wa marehemu Rugemarila Mutahaba," alieleza Mapunda katika ushahidi wake.

Alisema, wizara hiyo kupitia Clouds Media Group ilichukua hatua ya kuajiri wabunifu wa kujitegemea ili kutengeneza wimbo ambao utaunga mkono kampeni hiyo, wimbo ndiyo huo wa Nchi Yangu ulioimbwa na Tanzania All Stars.

Kesi hiyo itaendelea leo kwa shahidi huyo anayeongozwa na mawakili wanaoitetea DSTV, Simon Lyimo naThomas Mathias, kuulizwa maswali dodoso na mawakili wa Ditto, Ally Hamza na Elizabeth Mlemeta.

Pia shahidi mwingine wa DSTV, Johnson Mshana kutoa ushahidi wake.

Ditto alifungua kesi ya madai Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam mwaka 2020 akiomba iamuru Multi Choice Tanzania imlipe fidia ya Sh. bilioni sita kwa kutumia wimbo wa Nchi Yangu aliodai ni wake katika matangazo yao ya biashara bila ridhaa yake wakati wa Kampeni ya Fainali za AFCON mwaka 2019.

Pia ameiomba mahakama iamuru alipwe Sh. milioni 200 kutokana na madhara ya jumla, pia alipwe riba ya asilimia 25 tangu siku alipofungua shauri hilo akidai kampuni hiyo imemnyima fursa ya kunufaika na kazi yake.

Upande wa Ditto uliokuwa na mashahidi watano akiwamo Producer wa wimbo huo, Emma The Boy na meneja wake, Rodney Rugambo, umefunga ushahidi wao.

Nje ya Mahakama, mmoja wa mawakili wa Ditto, Elizabeth Mlemeta alisema, Jaji amekubali maombi yao baada ya kuondoa nyaraka ambazo zililetwa na DSTV nje ya taratibu za kisheria.

"Vielekezo vililetwa nje ya muda, jaji amekubali maombi yetu hivyo nyaraka hizo hazitazingatiwa na Jumatano (leo) tutaendelea na maswali dodoso kwa upande wa shahidi wa DSTV," alisema Elizabeth.

## Yanga ilivyotwaa ubingwa 2023/24

INATOKA UK. 24

kuamua ubingwa kwa Yanga msimu huu ni dhidi ya Dodoma Jiji iliyochezwa Februari 5, mwaka huu ambapo ilipata ushindi kwa mbinde bao 1-0 na siku tatu baadaye ilipoichapa Mashujaa FC magoli 2-1, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Februari 11, mwaka huu iliwachapa Prisons mabao 2-1, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya.

Kwa kiasi kikubwa hizi ndizo mechi zilizoamua ubingwa, na zilizofuata ilionekana kama ni kukamilisha ratiba, ambapo mashabiki wengi walichokuwa wakisubiria timu hiyo itatwaa ubingwa lini na kabla ya mechi gani kwa sababu tayari ilikuwa imeziacha Simba na Azam kwa tofauti kubwa ya pointi.

Hata hivyo, mechi hizo za Yanga zilirahisishwa zaidi na mechi ambazo Simba na Azam zilishindwa kasi ya kukimbizana na mabingwa hao.

Simba ilionekana kuisaidia Yanga kutwaa ubingwa ilipotoa sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo Novemba 9, mwaka jana na sare ya mabao 2-2 dhidi ya timu hiyo hiyo waliporudiana Aprili 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.

Sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC, Desemba 23, mwaka jana pia iliipoteza Simba katika mbizo na kuibeba Yanga, sare ya bao 1-1 dhidi ya Ihefu na kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Prisons lakini pia suluhu dhidi ya Kagera Sugar pia iliwarahisishia kazi kwa mabingwa hao.

Azam nayo ambayo ilijinasibu msimu huu kutwaa ubingwa, iliathiriwa na suluhu dhidi ya Dodoma Jiji, kipigo cha mabao 3-2 dhidi ya Yanga, kipigo kingine cha nyumbani cha mabao 3-1 dhidi ya Namungo, sare ya bao 1-1 dhidi ya Simba, Februari 9, mwaka huu, zikifuatia zingine dhidi ya Coastal Union, Prisons, kabla ya kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Simba, Mei 9, mwaka huu, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, kilizima ndoto za kutwaa taji hilo na Yanga ikachukua ubingwa kabla ya mechi tatu Ligi Kuu msimu huu kumalizika.

Yanga imetwaa ubingwa mara ya tatu mfululizo, ikiwa ni mara ya nne katika historia ya soka nchini kufanya hivyo.

Ilifanya hivyo mwaka 1991, hadi 1993, ikatwaa tena mara tatu mfululizo mwaka 1996 hadi 1998, ikarudi tena msimu wa 2014/15, hadi 2016/7, na hii ni mara ya nne, kuanzia 2021/22.

Timu hiyo pia ina rekodi ya kutwaa mara tano mfululizo kuanzia mwaka 1968 hadi 1972, kama ilivyokuwa na watani zao wa jadi, Simba ambao walifanya hivyo mara tano pia kuanzia mwaka 1976 hadi 1980.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliliambia gazeti hili timu hiyo itakabidhiwa Kombe la Ubingwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa baada ya kuwakaribisha Tabora United, ambapo wachezaji wa timu pinzani watasimama kwa ajili ya ‚paredi' maalumu kabla ya mechi hiyo kuanza.

Hiyo itakuwa kabla ya mechi yao ya kumaliza msimu ambayo itachezwa Mei 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex dhidi ya Prisons.

Michezo
Jumatano Mei 22, 2024
Nipashe

## Raya: Ninataka kubaki Arsenal

UKURASA 21



# YANGA ILIVYOTWAA UBINGWA 2023/24

**●●●Ni pale ilipoichapa Simba nje na ndani, Azam huku klabu hizo...**

**Na Adam Fungamwango**

YANGA imefanikwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ikiwa ni mara ya tatu mfululizo kuanzia msimu wa mwaka 2021/22 na imebakiwa na mechi tatu mkononi.

Ubingwa huo ni wa 30 kwa Yanga, katika historia yake, tangu ilipoanza kufanya hivyo kwa mara ya kwanza mwaka 1968.

Dalili za kutwaa ubingwa msimu huu kwa timu hiyo zilianza kuonekana mapema, kwa baadhi ya mechi zake ilizocheza na hata matokeo ya timu nyingine yalionekana kuwarahisishia kazi mabingwa hao.

Makocha wakubwa duniani, wanasema ili kutwaa ubingwa, kwanza inabidi timu inayousaka izifunge timu ambazo zinaonekana kugombea moja kwa moja taji hilo, au kupata pointi nyingi kutoka kwao.

Yanga ilionekana itakuwa mabingwa wa msimu huu mapema kuanzia Oktoba 23, mwaka jana ilipoichapa Azam FC mabao 3-2, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam licha ya kufungwa katika mechi ya marudiano iliyofanyika Machi 17, mwaka huu.

Baada ya Yanga kugawana pointi tatu na Azam, ikachukua pointi zote sita kutoka kwa watani zao Simba, hivyo ikawa imekusanya pointi tisa kati ya 12, kutoka kwa wapinzani wake wanaoonekana kutaka ubingwa huo.

Novemba 5, mwaka jana ilitoa kipigo cha mabao 5-1 dhidi ya Simba, kabla ya kushinda mechi ya mzunguko wa pili kwa mabao 2-1 mechi iliyochezwa Aprili 20, mwaka huu, katika michezo hiyo miwili ambayo ilionekana kuamua ubingwa kwa Yanga.

Mechi zingine ambazo zilionekana

INAENDELEA UK. 23




Wachezaji wa Yanga wakishangilia baada ya kufunga bao katika moja ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa mwaka 2023/2024 iliyochezwa hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

## Viwanja AFCON 2027 kukamilika mwakani

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa ujenzi wa viwanja vipya vya michezo kwa ajili ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027), vinatarajiwa kukamilika mwakani ili kupisha ukaguzi wa kikanuni utakaofanywa na maofisa wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma, amesema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza Mbunge wa Chake-chake, Ramadhan Suleiman Ramadhan, ambaye amehoji lini viwanja vipya ambavyo serikali inatarajia kujenga kwa ajili ya matayarisho ya AFCON vitakamilika.

Mwinjuma akijibu swali hilo, alisema kwa mujibu wa ratiba na mahitaji, viwanja hivyo vinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka ujao ili kupisha ukaguzi wa kikanuni wa CAF ambao utafanyika baada mwaka 2025.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Chumbuni, Ussi Salum Pendeza, amehoji ni lini serikali itaamua kuwekeza kwa nguvu zote katika viwanja, walimu na mawakala wa michezo mbalimbali inayoonekana kuleta tija kwa Taifa.

Akijibu swali hilo, Mwinjuma, alisema serikali inatekeleza ujenzi wa viwanja vya mpira wa miguu katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Zanzibar (Fumba), Ilemela jijini Mwanza pamoja na akademia na hosteli katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

CAF tayari imeshatangaza rasmi Tanzania, Kenya na Uganda zitakuwa wenyeji wa Fainali za AFCON zitakazofanyika mwaka 2027,

Nchi hizo tatu za Afrika Mashariki zimepata nafasi hiyo baada ya kupeleka maombi ya pamoja.

Hata hivyo, Tanzania pia inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazochezwa Septemba, mwaka huu.

Uwanja wa Benjamin Mkapa, Uhuru na Azam Complex, vinatarajiwa kufungwa ili kupisha maboresho kwa ajili ya kukidhi viwango vya mashindano hayo ya kimataifa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042